HALIUZWI

# Jarida la NEMC

BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

ISBN 0856 - 6933 | TOLEO NA. 007 | APRILI - JUNI, 2022

# WAZIRI MKUU ASISITIZA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI JIJINI DODOMA




Ndani:

- MRADI WA BOMBA LA MAFUTA NI SALAMA KWA MAZINGIRA - MKURUGENZI NEMC
- MHE. JAFO ATEMBELEA GHALA LA KUHIFADHIA NGOZI GHAFI TEMEKE
- **MAKALA:** UPANDAJI MITI KWA WINGI UTASAIDIA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

@nemctanzania

NemcTVTanzania

www.nemc.or.tz

#MazingiraYetuUhaiWetu

# YALIYOMO


| Na. | Maelezo | Uk |
|---|---|---|
| 1. | WAZIRI MKUU ASISITIZA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI JIJINI DODOMA | 3 |
| 2. | WAZIRI JAFO AZINDUA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA | 4 |
| 3. | WAZIRI BASHUNGWA AZINDUA WARSHA YA MAAFISA MAZINGIRA DODOMA | 5 |
| 4. | WAZIRI MKUU AHIMIZA UPANDAJI NA UTUNZAJI WA MITI KATIKA MJI WA SERIKALI MTUMBA - DODOMA | 6 |
| 5. | BODI YA WAKURUGENZI YA NEMC YAFANYA ZIARA - SGR | 7 |
| 6. | MAKALA: KELELE NI JANGA LINALOATHIRI VIUMBE HAI NA MAZINGIRA | 8 |
| 7. | MRADI WA BOMBA LA MAFUTA NI SALAMA KWA MAZINGIRA - MKURUGENZI NEMC | 9 |
| 8. | NEMC YASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI JUNI 2022 | 10 |
| 9. | DHANA YA UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA MAZINGIRA | 12 |
| 10. | TUNAPOADHIMISHA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI TUJITAFAKARI KUHUSU UTUNZAJI WA MAZINGIRA - MHE. JOKATE MWEGELO | 14 |
| 11. | NEMC KANDA YA MAGHARIBI YASHIRIKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA BIASHARA | 14 |
| 12. | MHE. JAFO ATEMBELEA GHALA LA KUHIFADHIA NGOZI GHAFI TEMEKE | 15 |
| 13. | MAKALA: UMUHIMU WA UPANDAJI MITI KATIKA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI | 16 |
| 14. | NEMC YATOA VIFAA NA KUSHIRIKI ZOEZI LA USAFI - KISUTU | 17 |
| 15. | NEMC YASHIRIKI ZOEZI LA KUFANYA USAFI KATIKA FUKWE ZA RAINBOW KAWE -JIJINI DAR ES SALAAM | 18 |
| 16. | MAKALA: GEREJI BUBU NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA NA AFYA YA JAMII | 19 |
| 17. | MAKALA: VIWANDA ENDELEVU, UCHUMI IMARA KWA MAZINGIRA SAFI NA SALAMA | 20 |
| 18. | MAKALA: IFAHAMU SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI TAREHE 5 JUNI KILA MWAKA | 21 |
| 19. | MAKALA: UMUHIMU WA UPANDAJI MITI KWENYE UHIFADHI WA MAZINGIRA | 22 |
| 20. | MAKALA: MADHARA YA MAFUTA NA MAFUTA MACHAFU KATIKA MAZINGIRA | 23 |
| 21. | KAULI YA MAZINGIRA | 24 |
| 22. | KAULI YA MAZINGIRA: KATUNI | 26 |


## UTANGULIZI

### BARAZA LA TAIFA LA HIFADHI NA USIMAMIZI WA MAZINGIRA (NEMC)

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilianzishwa kwa Sheria ya Taifa ya Usimamizi wa Mazingira Na. 19 ya mwaka 1983 kama chombo cha kuishauri serikali juu ya masuala ya utunzaji endelevu wa Mazingira. Baraza lilianza kazi rasmi mwaka 1986. Sheria Na. 19 ya mwaka 1983 ilifutwa mwaka 2004 na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Na. 20 ya mwaka 2004 (Sura 191) ambayo ilianzisha Baraza kwa mara nyingine.

Tangu kuanzishwa kwake, Baraza limekuwa likisimamia na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu suala zima la hifadhi ya mazingira na maendeleo endelevu nchini. Kwa mujibu wa kifungu cha 17 cha Sheria hiyo, madhumuni na sababu za kuanzisha Baraza hili ni kuratibu utekelezaji wa Sera na Sheria ya Mazingira katika nyanja kuu nne ikiwa ni pamoja na:-

1. Kutekeleza shughuli za uzingatiaji na utekelezaji (enforcement and compliance) wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira;
2. Kusimamia mchakato wa Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) (Kuratibu, kufanya mapitio ya ripoti za TAM kutoka kwa wenye miradi na kufuatilia utekelezaji wake);
3. Kufanya tafiti za mazingira;
4. Kuwezesha ushiriki wa umma katika kufanya uamuzi unaohusu mazingira na kusimamia kwa ujumla na kuratibu masuala yote yanayohusu Mazingira kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Sheria nyingine zozote zilizoandikwa.


**BODI YA UHARIRI:**

**Mwenyekiti:**
Dkt. Menan Jangu

**Mhariri Mkuu:**
Irene John

**Wachangiaji:**
Monica Sapanjo
Dalia Charles
Rose Mtui
Adam Sayi
Judith Mwakolo
Dkt. Befrina Igullu
Pendo Kundya
Neema Mdimi
Hilda F. Mwakasungura
Romanus Tairo

**Msanifu Michoro:**
Blasius Haule

# WAZIRI MKUU ASISITIZA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI JIJINI DODOMA

Watanzania wametakiwa kusitisha mara moja tabia ya utiririshaji wa maji machafu kutoka viwandani na kwenye migodi kwani inachangia kuhatarisha usalama wa afya ya binadamu na mazingira.

Kauli hiyo imetolewa na Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa alipokuwa akizungumza na wananchi pamoja na wadau wa mazingira wa Mkoa wa Dodoma katika kilele cha maadhimisho ya siku ya Mazingira duniani, mkutano uliofanyika katika ukumbi wa Jakaya Kikwete uliopo Mjini Dodoma.

Amesema utiririshaji holela wa majitaka na maji machafu ya viwandani ni hatari kwa afya ya binadamu kwani maji hayo yanaweza kubeba kemikali hatarishi kwa afya ya viumbe hai na mazingira kwa ujumla.

"Hivi karibuni tumeshuhudia kutoweka kwa baadhi ya viumbe hai, maeneo mengi ya vyanzo vya maji yameathirika kutokana na ukame wa mara kwa mara, uchafuzi wa mazingira unaotokana na majitaka na kemikali kutokana na shughuli za viwandani. Uchafuzi huu umeendelea kuongezeka kwa kasi nchini na kuathari maji, hewa na ardhi. Hali hii inahatarisha usalama wa afya ya binadamu na mazingira," amesema Mhe. Kassim Majaliwa

Aidha, amekemea tabia ya uchomaji miti, uvamizi na uharibifu wa mapori tengefu, ukataji wa miti holela kwa ajili ya uchomaji wa mkaa, uvamizi na uharibifu wa vyanzo vya maji pamoja na uchomaji moto misitu.




*Mhe. Kassim Majaliwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania akizindua Mpango kabambe wa Uhifadhi wa Mazingira kwenye kilele cha maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani yaliyoadhimishwa Kitaifa jijini Dodoma.*

"Kutokana na kuongezeka kwa uharibifu wa mazingira, ninaagiza Wizara na taasisi husika, pamoja na wananchi kwa ujumla, kuimarisha ushirikiano katika kukomesha uvamizi na uharibifu wa mapori tengefu kote nchini. Ninawasihi wananchi tutoe ushirikiano wa kutosha kuhakikisha tunarejesha misitu, ikolojia na uoto wa asili katika maeneo yetu, hususan maeneo ambayo miti ya asili iko kwenye tishio la kutoweka. Tuwe walinzi wazuri wa mazingira kwa faida ya kizazi hiki na kijacho,"

Pamoja na hayo Waziri Mkuu amezindua mpango kabambe wa uhifadhi wa mazingira na kutoa maagizo 15 kwa wizara, taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu uhifadhi wa mazingira nchini na kutaka yatekelezwe kikamilifu na kuzindua Mpango kabambe wa uhifadhi wa mazingira.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamiu wa Rais anayeshughulikia mazingira, Dkt. Suleiman Jafo amesema ofisi yake imezindua mpango wa soma na mti ambapo kila mwanafunzi anapaswa kupanda mti mmoja.

"Tumezindua kampeni ya Soma na Mti ambapo wanafunzi milioni 14.5 kutoka shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu wameshiriki kwa kupanda mti mmoja mmoja.

Katika hatua nyingine Mhe. Kassim Majaliwa ametoa tuzo kwa Mabalozi wa Mazingira na viongozi wakuu wa Nchi watano akiwemo Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan.

# WAZIRI JAFO AZINDUA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo alipanda mti katika kwenye eneo la Iyumbu Park katika uzinduzi wa wiki ya Maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani iliyoadhimishwa Kitaifa jijini Dodoma.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo amezindua maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani yanayofanyika Kitaifa jijini Dodoma kuanzia tarehe 28 Juni hadi kufikia kilele chake tarehe 5 Juni 2022.Katika uzinduzi huo Mhe. Waziri alifanya matembezi na kushiriki katika zoezi la kupanda miti katika eneo la Iyumbu Mkoani humo.

Dkt. Jafo ametoa pongezi kwa Mkuu wa Mkoa wa Dodoma pamoja na wananchi kwa kushiriki kikamilifu kwenye utunzaji wa mazingira kwa kupanda miti katika maeneo mbalimbali. Pia amesisitiza kuongeza juhudi za kuhifadhi mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa kila mmoja kupanda miti na kuitunza kwa maendeleo endelevu. Amezitaka taasisi mbalimbali kama shule, vyuo, hospitali, magereza na maeneo mbalimbali kupanda miti na kufanya usafi ili kudumisha usafi na uhifadhi wa mazingira.

Amesema "mabadiliko ya tabianchi yamekuwa na changamoto kubwa duniani, suala la ukame maeneo mbalimbali na mvua zisizotosheleza, jambo la kufanya ni kila mwananchi kufuata ajenda ya utunzaji wa mazingira na upandaji miti ili kufikia lengo la kupanda miti millioni 276 kwa mwaka ili kuongoa mfumo ikolojia." Pamoja na hayo amewaomba wananchi kujitokeza katika viwanja vya Jakaya Kikwete katika maonesho ya maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani kuanzia tarehe 1 hadi kilele tarehe 5 ili kujifunza teknolojia mbalimbali za kuhifadhi mazingira kwa maendeleo endelevu.



# WAZIRI BASHUNGWA AZINDUA WARSHA YA MAAFISA MAZINGIRA DODOMA




Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI Mhe. Innocent Bashungwa amezindua rasmi Warsha ya Maafisa Mazingira iliyojumuisha Maafisa mazingira wa ngazi ya Kitaifa, Mkoa na Wilaya. Warsha hiyo iliendeshwa katika ukumbi wa Chuo cha Mipango jijini Dodoma na kuhudhuriwa na viongozi mbalimbali.

Akifungua warsha hiyo Mhe. Bashungwa amesema " Suala la utunzaji wa mazingira na mikakati endelevu ya utunzaji wa mazingira ni jambo letu sote sambamba na kutoa elimu kwa umma kwa kuzingatia uhitaji wa uchumi wetu." Amewasihi watanzania wote kutunza mazingira kwani ni jukumu la kila mmoja na si la Maafisa mazingira pekee.

Aidha amesisitiza umuhimu wa kutoa mafunzo kwa Maafisa mazingira ili kuwajengea uwezo wa kutoa elimu iliyo sahihi kwa jamii juu ya utunzaji wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo kusaidia kupunguza athari za mazingira na kukuza uchumi wa Taifa kwa maendeleo endelevu.



**Mhe. Innocent Bashungwa**
*Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais TAMISEMI*



*Watumishi wa NEMC pamoja na maafisa mazingira wa Wilaya, Mkoa na Kitaifa washiriki Warsha ya Maafisa Mazingira jijini Dodoma.*

# WAZIRI MKUU AHIMIZA UPANDAJI NA UTUNZAJI WA MITI KATIKA MJI WA SERIKALI MTUMBA - DODOMA



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akipanda mti kwenye uzinduzi wa zoezi la upandaji miti katika eneo la mji wa Serikali Mtumba Dodoma.*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa amewaongoza wakazi wa Dodoma katika uzinduzi wa zoezi la upandaji miti katika mji wa serikali Mtumba. Katika katika hafla hiyo ya uzinduzi ameambatana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo pamoja na viongozi mbalimbali wa Kitaifa na Mkoa na Wilaya.

Mhe. Majaliwa amesema Serikali kupitia Ofisi ya Rais ikishirikiana na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira imeendelea kuratibu utekelezaji wa kampeni ya kitaifa ya upandaji na utunzaji wa miti inayotekelezwa nchini kwa kila Halmashauri kupanda miti milioni 1.5 kila mwaka.

Amesema "suala la kupanda miti na kuitunza ni la muhimu kwa ustawi wa Mazingira ya Taifa letu hatua inayokwenda sambamba na kuhimili mabadiliko ya tabianchi lakini pia kuwezesha mazingira ya Miji yetu kuwa ya kijani na mandhari nzuri ya kuvutia.

Sambamba na hayo Mhe. Majaliwa ameagiza Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira, timu ya wataalamu pamoja na Wakala wa Huduma za Misitu kusimamia kikamilifu ujenzi wa mji wa serikali, programu ya upandaji miti pamoja na kuelimisha jamii juu ya upandaji bora wa miti kwa kuzingatia hali ya hewa ya eneo husika ili upandaji uwe na tija.

# BODI YA WAKURUGENZI YA NEMC YAFANYA ZIARA - SGR

BODI ya Wakurugenzi ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC), imefanya ziara katika mradi wa Reli ya Kisasa (SGR) na kushauri masuala mbalimbali ya mazingira.

Hatua hiyo ya Bodi ya NEMC ni utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Bunge, Uwekezaji, Viwanda na Mazingira ambapo waliagiza miradi ya Kimkakati inapojengwa Baraza lifuatilie kwa karibu badala ya kusubiri athari zitokee ndio hatua zichukuliwe.

Akizungumza katika ziara hiyo ya ukaguzi kutoka Dar es Salaam hadi Ruvu, Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Prof.Esnath Chaggu, amesema wamefika kukagua uzingatiaji wa masuala ya mazingira katika mradi huo mkubwa na muhimu kwa Taifa.

"Usafirishaji kwenye nchi yetu ni suala muhimu sana ndiyo maana mradi huu mkubwa umeanzishwa, kwa taarifa tulizozipata uzingatiaji wa masuala ya mazingira unafanyika vizuri na wanafuatilia kwa ukaribu." alisema.

Naye, Mkurugenzi Mkuu wa NEMC, Dkt. Samuel Gwamaka, alisemaziara hiyo ni utekelezaji wa maagizo ya kamati hiyo ili kuepuka athari za kimazingira kutokana na mradi huo."Hata Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan amekuwa akisisitiza miradi hii mikubwa ya maendeleo sisi Baraza tuwe karibu nayo kufanya ufuatiliaji ili kushauri pale ambapo patakuwa na changamoto ya Kimazingira." alisema.



*Bodi ya Wakurugenzi ya NEMC wakiwa kwenye picha ya pamoja na wakandarasi wanaojenga reli ya kisasa (SGR) walipofanya ziara kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira katika mradi huo.*

Alibainisha kuwa katika ziara hiyo wamezungumza na Menejimenti ya Shirika la Reli Tanzania (TRC) ambapo miongoni mwa mambo yaliyozungumzwa ni kero ambayo wananchi wamekuwa wakiipata wakati wa ujenzi ikiwemo eneo la Kipawa kuwa na mafuriko na baadhi ya meneo kutokuwa na vivuko hivyo wananchi kulazimika kutembea umbali mrefu wanaphitaji kuvuka kwenda upande mwingine.

"Tumeshauriana jinsi ya kuchukua hatua mbalimbali ili kuondoa malalamiko hayo na tayari kwenye baadhi ya maeneo tayari wameanza ujenzi wa vivuko." alisema.

Dkt. Gwamaka alimalizia kwa kuwapongeza TRC jinsi walivyozingatia masuala mazima ya utunzaji wa mazingira kwa ajili ya maendeleo endelevu wa nchi yetu.

Bodi ya Wakurugenzi ya NEMC ni mara yao ya kwanza kufanya ziara katika mradi huo ambao ni mkubwa na wa kimkakati, Bodi hiyo itaendelea kufuatilia kwa ukaribu namna utekelezwaji wa Sheria ya Mazingira unavyofuatwa ili kuepuka athari zinazoweza kujitokeza.



*Mkurugenzi wa NEMC Dkt. Samuel Gwamaka akipata maelezo kutoka kwa kiongozi wa usimamizi wa ujenzi wa reli ya kisasa (SGR) namna mradi huo unavyojengwa kwa kuzingatia utunzaji wa mazingira walipofanya ziara kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira katika mradi huo.*



*Mwenyekiti wa Bodi ya NEMC Prof. Esnath Chaggu (Wa pili kutoka kushoto - mbele) pamoja na Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Dkt. Samuel Gwamaka wakiwa kwenye picha ya pamoja na wakandarasi wanaojenga reli ya kisasa SGR walipofanya ziara ya kukagua mazingira kwenye mradi wa reli hiyo.*

# KELELE NI JANGA LINALOATHIRI VIUMBE HAI NA MAZINGIRA



Uchafuzi wa mazingira utokanao na kelele imekuwa ni tishio kubwa kwa siku za hivi karibuni.. Ni ukweli usiopingika kuwa kelele zinasababishwa na shughuli mbalimbali za viwanda, mipango isiyo endelevu ya miji kama kumbi za starehe na burudani, nyumba za ibada kuwa karibu na makazi ya watu, shughuli za kijamii kama harusi, sherehe, matamasha yakiwa yameambatana na matumizi ya vipaza sauti vyenye sauti ya juu. Kelele ni sauti zilizozidi kiwango kilichoruhusiwa na chenye kusababisha madhara kwa afya ya binadamu, Wanyama na mazingira. Uchafuzi wa mazingira unaotokana na kelele unasababishwa na uachiliaji kelele zisizozuilika au kudhibitiwa pale zinapozalishwa na kusababisha athari za kiafya kwa jamii

Aidha uchafuzi huu wa mazingira utokanao na kelele unasababishwa pia na uelewa mdogo wa jamii kuhusu uwepo wa kanuni na sheria zinazozuia usumbufu wowote kwa watu wengine . Kwa mujibu wa Katiba ya Nchi, na Sheria ya Mazingira yam waka 2004, kila mwananchi ana haki ya kuishi katika mazingira safi na salam. Pia Suala la udhibiti wa kelele limetiliwa mkazo katika Sheria nyingine mbalimbali. Mfano katika Sheria ya Afya ya Jamii ya mwaka 2009 kifungu cha 53 (W) ambacho kinataja kelele kama mojawapo ya kero (Nuisance). Sanjari na kifungu 53, vifungu 54 - 60 vinatoa nguvu kwa mamlaka (LGA), Mganga Mkuu Mkoa, Mganga Mkuu wa Wilaya na Afisa Afya Mazingira ambao ni "Authorized officers" kuingia na kukagua jengo lolote, kuondosha chukizo, au hatari, kutoa ilani au maelekezo, kufunga biashara au huduma iliyo na usumbufu wa kelele kwa jamii. Katika Sheria ya Mpango Mji ya mwaka 2007, udhibiti wa kelele umepewa umuhimu kwa kuandaa kanuni zinazoelekeza uendelezaji ardhi kufanyika kwenye maeneo yaliyotengwa kutokana na aina ya shughuli. Aidha Kanuni ya 7 (3) ya Kanuni za Mipangomiji (Maombi ya Idhini ya Uendelelezaji) za Mwaka 2018 inaelekeza kuhakikisha uendelezaji wowote unaofanywa hauleti kero yoyote (ikiwemo kelele) inayoweza kuhatarisha afya ya jamii. Sheria ya Jumuiya [Sura ya 337 Marejeo ya 2002] imeangalia Usalama wa wananchi na kuzitaka jumuiya zote za dini zilizosajiliwa kutunza amani miongoni mwao na kwa jamii nzima. Kifungu cha 14(a) sheria ya Jumuiya Sura 337 kinazitaka jumuiya zote za dini nchini kuzingatia sheria mbalimbali zilizopo nchini. Kukosekana kwa uelewa wa Sheria na kanuni zinazodhibiti uchafu wa mazingira unaotokana na kelele, kumepelekea ukiukwaji na hivyo kuleta kero kwa jamii.

Hivyo tutafakari kwa kina juu ya madhara yatokanayo na kelele kwenye makazi zinazosababishwa na Viwanda vilivyojengwa kwenye maeneo ya makazi, vyombo vya usafiri sambamba na maendeleo ya teknolojia tuliyonayo. Kuongezaka kwa matumizi ya vipaza sauti vya kisasa vinavyotumika katika kumbi za starehe, nyumba za ibada na maeneo ya wazi kumechangia kuongezeka kwa kelele zilizopitiliza viwango vilivyoruhusiwa.

Kuna athari nyingi za uchafuzi wa mazingira zitokanazo na kelele zimezidi kukua kwa kasi zaidi ikiwa na madhara mengi zaidi siku za hivi karibuni, athari zake zikiwa kiafya Zaidi kama kupunguza uwezo wa usikivu, kusababisha ulemavu kama uziwi, upungufu wa uwezo wa kuzaa unaosababishwa na stress, huharibu uwezo wa kujifunza, husababisha utoro, hupelekea ongezeko katika matumizi ya madawa kujitibu, huweza kusababisha ajali, kelele huingilia uwezo wa kawaida wa kuzungumza na kusababisha ulemavu na mabadiliko ya tabia.

Aidha kelele kwa namna nyingine husababisha udhia, uchovu na msongo, kutokuwa na uhakika, kutojiamini, maudhi, kutokuelewana, uwezo mdogo wa kufanya kazi, kuharibu uhusiano na maelewano, Usumbufu wa usingizi ambapo hali hii husababisha kuwa na shinikizo la damu, mapigo ya moyo yasiyo ya kawaida hutokea (haraka au polepole), Hupelekea kuwa na uchovu, huzuni na kupunguza uwezo wa kufanya kazi, Usumbufu wa mishipa ya moyo na kusababisha magonjwa ya moyo kutokana na msongo wa muda mrefu, Kelele za papo hapo au muda mrefu na kwa kiwango cha juu hushtua neva na homoni hivyo kupelekea shinikizo la damu shubiri

Kuathirika kwa akili na kusababisha wasiwasi, msongo, hofu, kichefuchefu ni athari nyingine ya afya ya binadamu vikiambatana na maumivu ya kichwa, ubishi, mabadiliko ya hisia kwenye tendo la ndoa, kuongezeka kwa migogoro ya kijamii, ugonjwa wa neva, ugonjwa wa "hysteria", na ugonjwa wa "psychosis", Kuharibika kwa utendaji wa kazi kwa kuongezeka makosa, kupungua kwa motisha kuathiri usomaji, kushindwa kukabiliana na kutatua matatizo na kupoteza kumbukumbu ,Kuharibika kwa utendaji wa kazi kwa kuongezeka makosa, kupungua kwa motisha kuathiri usomaji, kushindwa kukabiliana na kutatua matatizo na kupoteza kumbukumbu zikiwa ni athari za kelele kwenye afya ya binadamu pia.

Kwa upande mwingine kelele zinaweza kuwa sababu kubwa ya ndege kuhamisha makazi yao au wanyama kutoka kwenye maeneo yao waliyozoea kuishi na kuzuia kuzaliana kwao, Wanyama na ndege hupata wasiwasi na hofu na hivyo kuathiri ukuaji na kuzaliana na wengine kufa.

Kutokana na athari nyingi zilizoainishwa hapo juu za kiafya ya binadamu, wanyama na ndege Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) lilifanya ukaguzi wa mazingira katika maeneo mbalimbali na kuibua changamoto kama mabadiliko ya matumizi ya ardhi yamekuwa yakiruhusiwa bila kufuata utaratibu wa kushirikisha jamii husika, kuruhusu mabadiliko ya matumizi ya ardhi kwa kipande cha ardhi kilichopo katikati ya makazi kumesabisha shughuli zenye kelele kuhamia kwenye makazi ya watu na hivyo kuleta malalamiko mengi; vibali vya shughuli za kumbi vimetolewa pasipokuzingatia masharti ya eneo husika; kiwango kidogo cha uelewa wa masuala ya mazingira kwa jamii; kukosekana kwa mipango ya usimamizi wa mazingira katika halmashauri na sekta; na ushirikiano mdogo wa wadau katika shughuli za hifadhi ya Mazingira.

Inaendelea Uk. 20 ...

# MRADI WA BOMBA LA MAFUTA NI SALAMA KWA MAZINGIRA - MKURUGENZI NEMC




*Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Dkt. Samuel Gwamaka akizungumza kwenye mkutano na waandishi wa habari kuhusu bomba la mafuta leo jijini Dar es salaam.*

Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Mhandisi Dkt. Samuel Gwamaka ameitisha mkutano na waandishi wa habari kuhusu suala la baadhi ya wanaharakati kutoka Mataifa mbalimbali kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kupinga ujenzi wa bomba la Mafuta linalotoka Hoima nchini Uganda hadi Chongoleani Mkoani Tanga.

Akiongea na waandishi wa habari Dkt. Gwamaka ametolea ufafanuzi suala la baadhi ya wanaharakati kupinga ujenzi wa bomba hilo kwa madai ya kuwa ujenzi huo una athari kwa mazingira. Ujenzi wa bomba hilo unaoendelea unatarajiwa kupita katika Mikoa nane na Wilaya ishirini na nne hadi kufika mwisho wa bomba hilo Chongoleani Tanga ambapo itajengwa bohari ya kuhifadhia Mafuta na miundombinu ya kujazia Mafuta kwenye Meli.

Dkt Gwamaka alisema "Baraza limehakikisha kwamba mradi huu wa bomba la mafuta ghafi Afrika Mashariki umezingatia masuala yote ya hifadhi ya mazingira kabla na wakati wa utekelazaji wake. Mradi huu ulisajiliwa na Baraza mwezi Machi 2017 takribani miaka mitano iliyopita na Kampuni ya Total East Africa Midstream ambayo ndio mwekezaji wa mradi huu uliopewa namba ya usajili 6725 kwa ajili ya mchakato wa tathmini ya athari za mazingira."

Aidha Baraza lilihakiki andiko la tathmini na kubainisha kuwa linazingatia na kuweka mipango yote ya kudhibiti athari za mazingira na masuala ya kijamii pamoja na kushirikisha wadau muhimu katika mikoa na wilaya zote zinazopitiwa na bomba hilo. Pia taasisi zote za serikali na zisizo za kiserikali pamoja na wataalamu kutoka Baraza walihusika katika kupata maoni kuhusu mradi huu, ikiwemo kufanya ziara katika maeneo yote ya mradi kuanzia tarehe 2 hadi tarehe 14 February 2019 na kufanya mapitio ya tathmini ya athari za mazingira kwa awamu mbili.

Awamu ya kwanza ni kikao cha kupata maoni ya wadau wote kutoka ngazi ya Taifa hadi wilaya na awamu ya pili ni kikao cha kamati ya Ushauri ya wataalamu (advisory committee) mnamo tarehe 3 April 2019 kilichohusisha wataalamu kutoka NEMC, vyuo vikuu mbalimbali, washauri elekezi pamoja na wawakilishi wa mradi,ambapo baada ya kikao hicho mradi uliidhinishwa na Waziri mwenye dhamana ya Mazingira na kupata cheti tarehe 29 Novemba 2019.

Pamoja na hayo amesema Baraza limeridhishwa na hatua za utekelezaji wa mradi kwa kuwa umefuata sheria na kanuni zote za nchi zinazosimamia miradi ya maendeleo, mazingira na uwekezaji hivyo athari za mazingira zitokanazo na mradi huu zinaratibiwa kwa utaratibu husika ulioainishwa katika andiko la tathmini ya athari za mazingira. Hatua za awali za ujenzi zimehusisha kulipa kwa fidia wananchi wa maeneo ambayo mradi huu unapitia na Baraza linafuatilia kwa karibu utekelezaji wa suala hilo kwa kufanya ziara eneo la Chongoleani na kujadiliana kuhusu hatua za utekelezaji kama zilivoainishwa kwenye andiko hilo.

Hivyo Dkt Gwamaka amewahakikishia watanzania kuwa" bomba hili la mafuta litaleta manufaa kiuchumi katika nchi yetu na wote waliguswa na mradi huu haswa waliohamishwa katika makazi yao, hali zao za maisha kubadilika na kuwa bora zaidi kuliko hapo awali ikiwemo ujenzi wa nyumba bora na za kisasa kwa waliohamishwa, pamoja na kutoa ajira mbalimbali kwa watanzania". Pia amewaomba wananchi kupuuzia maneno ya wanaharakati wanaopinga ujenzi huu kwani bomba hili lina manufaa makubwa kwa Nchi na Afrika Mashariki wa ujumla.

# NEMC YASHIRIKI MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI JUNI 2022




*Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wakiwa kwenye picha ya pamoja katika banda la NEMC kweye wiki ya maadhimisho ya siku ya Mazingira 2022.*

Kila mwaka ifikapo mwezi Juni, Tanzania huungana na Nchi nyingine kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Lengo kuu la maadhimisho ya siku hii ni kukumbushana na kuhamasishana juu ya kuhifadhi na kutunza mazingira yetu ili yawe endelevu. Kwa mwaka 2022 Kitaifa shughuli za maadhimisho zilifanyika Jijini Dodoma yakiratibiwa na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira kwa kushirikiana na Uongozi wa Mkoa wa Dodoma. Kauli mbiu iliyobeba ujumbe wa mwaka 2022 ni ***"Tanzania Moja Tu, Tunza Mazingira"*** ukiwa na maana kuwa watanzania wote tunategemea Nchi yetu na Rasilimali zilizopo hivyo hatuna budi ya kuitunza Tanzania yetu na rasilimali zake kwa manufaa ya wananchi wote na kuwa na maendeleo endelevu.

Maadhimisho ya siku hiyo muhimu yaliambatana na shughuli mbalimbali zilizolenga kuhamasisha Utunzaji wa Mazingira kwa Watanzania kuanzia tarehe 28 Mei - 4 Juni, 2022. Shughuli hizo ni kama ifuatavyo; kufanya uzinduzi wa maadhimisho hayo kwa kufanya matembezi na kupanda miti katika eneo la Mtumba Jijini Dodoma, kufanya ziara katika Taasisi na maeneo mengine mbalimbali kuona namna wadau mbalimbali wanavyozingatia suala la utunzaji wa mazingira. Vilevile ziliandaliwa warsha kwa wadau mbalimbali wa mazingira na maafisa mazingira wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri zote Tanzania ili kuongeza uelewa kwa wadau kuhusu masuala ya mazingira kupitia mada mbalimbali zilizowasilishwa. Tarehe 5 Juni, 2022 ilikuwa ndiyo siku ya kilele cha maadhimisho hayo.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) kama mdau mkubwa wa kusimamia Sheria ya Mazingira na Kanuni zake lilishiriki kikamilifu katika shughuli zote zilizofanyika katika wiki ya maadhimisho na kupata fursa ya kuweza kutoa elimu ya utunzaji wa mazingira kwa umma. Pia wananchi walipata fursa ya kulijua Baraza pamoja na majukumu yake. Vilevile wananchi waliweza kutoa malalamiko yao kuhusu kero mbalimbali za kimazingira na kujua namna ya kusajili miradi kwa njia ya kielektroniki.

Kupitia warsha iliyoandaliwa kwa Maafisa Mazingira wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri, Baraza lilipata fursa ya kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji, maeneo oevu na Tafsiri ya Sheria ya Mazingira namba 20 ya mwaka 2004. Sambamba na hilo, na kama Taasisi, Baraza lilifanikiwa kushiriki katika ziara zilizofanyika katika maeneo mbalimbali ndani ya Mkoa wa Dodoma ili kuona namna wadau mbalimbali wanavyotunza mazingira kama vile kupanda miti, udhibiti wa taka ngumu, taka maji na taka hatarishi.

### Uzindizi wa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani

Siku hii iliambatana na matembezi ya kuhamasisha jamii katika suala zima la kutunza mazingira na kupanda miti katika eneo la Mtumba. Miti takribani mia mbili (200) ilipandwa siku hiyo, na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo alitoa agizo la kuitunza na kuilinda kikamilifu miti hiyo ili kuhakikisha inamea na kukua. Vilevile, Mhe. Waziri aliwahamasisha wananchi kuendelea kupanda miti kwa wingi ili kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

### Uzinduzi wa Upandaji miti katika eneo la Mji wa Serikali Mtumba

Maadhimisho ya siku hiyo yaliambataba na Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa kuzindua rasmi zoezi la upandaji miti katika Mji wa Serikali Mtumba (Magufuli Government City), eneo ambalo linatarajiwa kupandwa miti takribani elfu tano (5,000) kwa ajili ya kujenga ikolojia stahimilivu kwa ajili ya kukabiliana na changamoto mbalimbali za kimazingira. Katika hotuba yake, Mhe. Waziri Mkuu alitoa wito kwa wananchi wote kulipa uzito unaostahili suala la kupanda miti na na kuwataka wananchi kushiriki kikamilifu katika kupanda miti na kuitunza kwa maendeleo ya nchi na ustawi wetu na vizazi vijavyo.

Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa akizindua zoezi la kupanda miti katika Mji wa Serikali Mtumba ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani

### Ziara katika Hospitali ya Benjamini Mkapa Dodoma

Katika eneo la hospitali ya Benjamini Mkapa, kulikuwa na mfano wa kuigwa katika suala zima la utunzaji wa mazingira. Hii ni kwa sababu uongozi umejikita katika matumizi ya nishati

mbadala ya gesi, uwepo wa mfumo maalumu wa kutibu majitaka (waste stabilization ponds), mfumo maalumu wa kudhibiti taka ngumu na taka hatarishi (incinerator) zinazotoka hospitalini hapo. Sambamba na hilo wamepanda miti ya kutosha ya matunda, kivuli na mapambo na wanaendelea kupanda miti hiyo katika maeneo jirani ambayo yapo wazi.

**Ziara eneo la Soko la Majengo Dodoma.**

Katika soko la Majengo ilionekana wadau wanajitahidi katika suala la usafi na udhibiti wa taka ngumu. Changamoto zilizobainika ni pamoja na uhaba wa vifaa vya kukusanyia taka na ufinyu wa eneo la kufanyia biashara. Hali hiyo ilipelekea Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Bi. Marry Maganga kuwataka viongozi wa soko kuhakikisha wanapata vifaa kwa ajili ya kukusanyia takataka na wafanyabiashara kuzingatia suala la usafi wa mazingira kama hatua itakayowasaidia kulinda afya zao.

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais -TAMISEMI Bw. Ramadhani Kailima alitoa wito kwa viongozi wa soko kuwa na vikao vya mara kwa mara vyenye ajenda ya kujadili mikakati kutunza mazingira. Bw. Kailima pia alielekeza viongozi kugawa maeneo ya soko ili kurahisisha shughuli za usimamizi wa mazingira na usafi.

Ziara Chuo Kikuu cha Mipango Dodoma

Wadau wa Chuo Kikuu cha Mipango walionesha jitihada kubwa katika swala zima la utunzaji wa mazingira na udhibiti wa taka ngumu. Aidha jitihada zinazofanyika katika chuo hicho ni pamoja na uanzishaji wa mradi wa kutenganisha taka ngumu. Aidha, uongozi umefanya utafiti kujua kiwango cha chakula kinachotolewa chuoni hapo kama kinatosheleza. Aidha, wadau wamepanda miti ya kutosha na wanaendelea kupanda ikiwa ni jitihada za kuifanya Tanzania ya kijani na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

**Warsha kwa Wadau wa Mazingira na Maafisa Mazingira wa Mikoa,Wilaya na Halmashauri**

Warsha hii ililenga kuwapa uelewa wadau wa mazingira kuhusu vipaumbele vya Ofisi ya Makamu wa Rais na wajibu wa COS's katika suala zima la hifadhi ya mazingira ikiwa ni pamoja na kuainisha vipaumbele kwa wadau wa maendeleo katika hifadhi ya mazingira. Pia warsha kwa maafisa Mazingira ililenga kuwapitisha wataalamu hao katika Sera ya Mazingira ya mwaka 2022; mikakati ya Utunzaji wa vyanzo vya maji na maeneo oevu; na Sheria ya Mazingira Namba 20 ya mwaka 2004. Kupitia warsha hiyo wataalamu wa mazingira wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri walipata fursa ya kusema mikakati ya utunzaji wa mazingira katika maeneo

*Inaendelea Uk. 13 >>>*



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo alipanda mti katika kwenye eneo la Iyumbu Park katika uzinduzi wa wiki ya Maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani iliyoadhimishwa kitaifa jijini Dodoma.*

*... Inatoka Uk. 19*

## KELELE NI JANGA LINALO ...

Aidha kwa kutambua umuhimu wa udhibiti wa kelele Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa mazingira (NEMC) lina dhamana ya kudhibiti kelele kupitia kanuni na sheria zilizopo. Kifungu cha 106 (5) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira yam waka 2004 kinakataza kupiga kelele kinyume na Kanuni za Mazingira za udhibiti wa Kelele na Kifungu cha 106 (6) cha Sheria hii kinaweka kosa la kupiga kelele bila kuzingatia maelekezo yaliyotolewa kwenye Kanuni.

Kanuni za usimamizi wa mazingira (Udhibiti wa kelele na mitetemo) za mwaka 2015 zimeanisha viwango vinavyotakiwa katika maeneo ya makazi, biashara, viwanda na hospitali kwa afya ya jamii. Viwango hivyo vinatofautiana kwa usiku na mchana (Mchana ni kuanzia saa 12 asubuhi mpaka saa nne usiku) na usiku (saa nne usiku hadi saa kumi na mbili asubuhi. Usiku viwango viko chini zaidi kwa kuwa ni muda ambao jamii inahitaji kupumzika. Viwango vinavyo ruhusiwa ni kama ifuatavyo;

| Kituo | dBA Mchana | dBA Usiku |
|---|---|---|
| Hospitali, Maktaba, Nyumba ya Wazee | 45 | 35 |
| Jengo la Makazi | 50 | 35 |
| Makazi mchanganyiko wa Biashara na burudani | 55 | 45 |
| Makazi na viwanda vidogo | 60 | 50 |
| Eneo la viwanda | 70 | 60 |

Pamoja na kuwepo kwa kanuni za mazingira za kudhibiti uchafuzi wa mazingira kwa kelele na mitetemo, bado hali hiyo inaendelea katika baadhi ya maeneo nchini.

Aidha Sheria na miongozo hiyo juu ya udhibiti wa kelele kwa kuzingatia changamoto hizo suala la udhibiti wa kelele lilipewa umuhimu wake na liliwekwa na kuelekezwa kwenye Sheria. Hivyo basi kila mtu au Taasisi anawajibu wa kufanya shughuli zake kwa kuzingatia sheria na miongozo ya nchi. Pia uendelezaji wowote wa ardhi ni muhimu kuhakikisha unakuwa na mifumo madhubuti ya kimazingira ya usimamizi wa Mazingira na kwa shughuli zinazopelekea kuzalisha kelele ni muhimu kuwa na vithibiti kelele (Sound Proof) pamoja na kuwa na kifaa cha kupimia sauti ili kuhakikisha kuwa shughui hiyo haileti usumbufu kwa jamii. , Pia mawasiliano baina ya taasisi ni muhimu sana ikiwa ni pamoja na kushirikiana kwa pamoja kuhifadhi na kulinda mazingira kwa ustawi wa Maisha ya jamii, kukuza uelewa kwa jamii kwenye masuala ya mazingira na mwisho kuna umuhimu wa kuzijengea uwezo taasisi au watu binafsi ili kuhakikisha usimamizi madhubuti wa masuala ya mazingira unafanyika.

# DHANA YA UZINGATIAJI NA UTEKELEZAJI WA SHERIA YA MAZINGIRA

Kwa miaka mingi duniani kote Sheria za mazingira zimekuwa zikitumiwa na Serikali katika kulinda na kuhifadhi mifumo ya hewa, maji, viumbe hai, udongo na afya za jamii. Hali kadhalika, Tanzania pia imekuwa ikitumia Sheria za mazingira namba 20 ya mwaka 2004 kuzuia utiririshaji wa maji taka kwenye mazingira, kulinda mimea na viumbe hai, kuzuia utupaji wa taka hatarishi na kemikali, kuzuia uchafuzi wa hewa, kelele na mitetemeko na kuhakikisha vyanzo vya maji vinaendelea kuwa safi na salama kwa jamii.

Hata hivyo, kuwa na Sheria ya mazingira pekee haitoshi kupunguza hizi changamoto za kimazingira. Ndio maana Serikali lazima ihakikishe kuwa shughuli za kijamii zinafikia matakwa ya Kisheria yaliyoainishwa kwenye Sheria Mazingira ya mwaka 2004 na Kanuni zake. Serikali kupitia Baraza la Taifa na Hifadhi wa Mazingira (NEMC) inakuwa na idara yenye mikakati endelevu ya kuhimiza na kulazimu shughuli za uchafuzi kuzingatia viwango vya kimazingira vinavyotakiwa. Hivyo, makala hii inatoa muhtasari wa msingi wa dhana zinazopelekea kuwa na mafanikio ya utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya mazingira.

Uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ya mazingira ni sehemu ya mpango endelevu wa shughuli za Baraza za kila siku katika kuhifadhi na kusimamizi wa mazingira ya umma. Mpango huu unaaanza pale ambapo umma unatambua kuwa kuna shida ya kimazingira na Serikali huchukua hatua katika kushughulikia shida hizo. Serikali imetengeneza Sheria na Kanuni za kuweza kutatua shida na changamoto za kimazingira lakini pia Baraza huandaa mpango wa kuweza kufikia malengo ya usimamizi wa Sheria. Ufuatiliaji na utekelezwaji wa Sheria unafanywa kwa kuzingatia misingi ya Sheria ya usimamizi wa mazingira ili kuhakikisha kuwa jamii iliyodhibitiwa inazingatia matakwa ya Kisheria. Baraza limelipa kipaumbele suala la utekelezwaji na uzingatiaji wa Sheria na kuhakikisha unakuwa endelevu kwa kujitathmini na kufanya marekebisho ya mara kwa mara ili kuboresha shughuli zake na kuhakikisha shughuli za jamii zinakuwa endelevu.

Baraza linatambua kuwa utunzaji wa mazingira ni kujumu la kila mwananchi, hivyo uzingatiaji na utekelezaji wa Sheria ili uwe endelevu unaanza kwa kuhakikisha kuwa jamii husika zimepewa elimu ya kutambua matatizo na changamoto za kimazingira zinazoweza kujitokeza katika maeneo yao. Miradi ya maendeleo na shughuli za kibinadamu zinapitia michakato ya Kisheria ya kutatua matatizo ya kimazingira ikiwa ni pamoja na kufanya Thathmini za Athari kwa Mazingira (TAM) na kufuata mifumo mbalimbali ya utunzaji wa mazingira. Mifumo ya utunzaji wa mazingira mara nyingi hufuatwa na wawekezaji kwa sababu wengine ni wapenzi wa kutunza mazingira, au ni mahitaji ya kibiashara na mwingine anafuata kwa sababu ni lazima afuate kama Sheria inavyotaka. Hivyo ni muhimu kujua aina ya wawekezaji wetu ili kuweza kusaidia kila mmoja kwa namna ya uwekezaji wake.



*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira Dkt. Seleman Jafo akiwa kwenye moja ya viwanda vinavyozalisha vinywaji nchini. Ziara hiyo ilikuwa na lengo la kufuatilia na kukagua utekelezaji wa Sheria ya mazingira.*

Ufuatiliaji na uzingatiaji wa Sheria ya mazingira ina manufaa kwa jamii, umma na wawekezaji. Hii inaonyesha umma utiii wa Sheria ya mazingira na utawala bora wenye kuleta usawa kwa wawekezaji wote. Lakini pia inaonyesha uimara wa taasisi kama chombo cha Kitaifa ambacho kimepewa dhamana ya kusimamia mazingira ili umma uendelee kunufaika na huduma zitokanazo na mifumo ya Kiikolojia na kulinda afya ya jamii. Hata hivyo, kwa wawekezaji hii inawapa motisha zaidi ya kuwekeza kwani hupunguza vihatarishi katika biashara zao kwa kuwa wabunifu zaidi na kuongeza ushindani unaotengeneza bidhaa bora na ajira endelevu.

Sheria ya mazingira imeweka mfumo wa utekelezaji wa Sheria kwa kutambua kuwa shughuli za maendeleo lazima ziwe endelevu, hivyo uchafu wa taka unaorudi katika mazingira lazima uwe katika kiwango kinachokubalika kwa kutoathiri mifumo ya ikolojia na afya ya jamii. Kuna viwango vya uchafuzi katika maji, kelele, udongo na hewa ambavyo shughuli za maendeleo lazima kuzingatia ili wasichafue mazingira. Ni wazi kuwa pale ambapo uwekezaji umefanyika kwa kuzingatia matakwa yote na miundominu sahihi imetumika, viwango vya kimazingira vinafikiwa katika uwekezaji wa aina zote. Pale ambapo viwango vinashidwa kufikiwa, Sheria ya mazingira ya mwaka 2004 inatoa uzingatiaji kwa kutumia hatua ambazo ni onyo au faini au kufunga na/au kuchukua hatua za kimashtaka. Ili kuhakikisha kunakuwa na mpango endelevu wa uzingatiaji wa Sheria ya mazingira ya mwaka 2004. Mwekezaji anapaswa kufanya Tathmini ya Athari kwa Mazingira (TAM) kabla hajawekeza. Hivyo mpango wa utunzaji wa mazingira utazingatiwa wakati wa ujenzi na uzalishaji wa mradi. Sheria pia inataka kuwa baada ya kuanza kufanya uzalishaji mwekezaji azingatie kufanya ufuatiliaji wa viwango vilivyowekwa kwenye mpango na kila mwaka aweze kuandaa taarifa ya kila mwaka ya kimazingira na kuiwasilisha Baraza. Jamii inajukumu la kutoa taarifa pale ambapo kunakuwa na hali ya uchafuzi wa Kimazingira. Lakini pia Baraza limejiwekea utaratibu kukagua athari za kimazingira kwa shughuli za kimaendeleo ili kuweza kusaidia kukidhi matakwa ya Sheria ya mazingira.

Pamoja na hatua zote hizi lakini bado kuna ukosefu wa uzingatiji na utekezaji thabiti wa Sheria ya mazingira. Hivyo Baraza linatoa rai kwa jamii, wawekezaji na mamlaka zingine kusaidia utunzaji na ulinzi wa mazingira kwa faida ya kizazi hiki na kijacho.

... Inatoka Uk. 11

wanayoyasimamia, na changamoto mbalimbali zinazowakabili katika kusimamia Sheria ya Mazingiara.

Lakini pia Mhe. Waziri alitoa maagizo 15 ya mikakati mbalimbali ambayo inatakiwa kutekelezwa ili kuleta matokeo chanya katika suala zima la kutunza mazingira. Maagizo hayo yalitolewa kwa Wizara mbalimbali, Mamlaka ya Serikali za Mitaa, Taasisi, Mashirika ya Serikali na binafsi na Sekta mbalimbali

**Maagizo hayo ni kama ifuatavyo:**

i. Wizara ya fedha na MipangoMpango Kabambe wa Usimamizi na Hifadhi wa Mazingira unapewa kipaumbele kwenye bajeti ya kila mwaka.

ii. Wizara za kisekta, Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuhakikisha Mpango Kabambe wa Hifadhi na Usimamamizi wa Mazingira unajumuishwa kwenye bajeti zao na kufuatilia na kuwasilisha taarifa ya utekelezaji,

iii. Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhakikisha maeneo yaliyoharibiwa yanarejeshwa kwa kupanda miti,

iv. Mamlaka ya Serikali za Mitaa ihakikishe inatekeleza program ya Kitaifa ya kupanda miti 1,500,000 ili kuhakikisha nchi yetu inakuwa ya kijani',

v. Wizara, Mashirika ya Serikali na binafsi yanayotumia nishati ya kuni na mkaa kupikia au shughuli nyingine ya uzalishaji zianze kutumia nishati mbadala,



Watumishi wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira wakimwagilia maji mti uliopandwa kwenye eneo la Iyumbu Park katika uzinduzi wa wiki ya maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani jijini Dodoma.

vi. Mamlaka za Serikali zihakikishe shughuli za uchomaji moto hovyo misitu inadhibitiwa.

vii. Taasisi za utafiti na vyuo vya elimu ya juu ziendelee kufanya tafiti za nishati mbadala kuondokana na utegemezi wa nishati ya kuni

viii. Kila Mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka utaratibu wa kuhakikisha taka zinatenganishwa na zinakusanywa,

ix. Mamlaka zinazohusika na usimamizi wa mifereji ya maji ya mvua mijini kuhakikisha mifereji hiyo inasafishwa ili kupunguza matukio ya mafuriko mijini;

x. Kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa ihakikishe maeneo yaliyotengwa kwa matumizi ya misitu ya mijini katika mamlaka zao hayabadilishwi matumizi wala kuvamiwa;

xi. Sekta zinazohusika zihakikishe kuwa ardhi na uoto hususan wa asili katika vyanzo vya maji, vilima na milima iliyo katika maeneo yao inalindwa na kuhifadhiwa ili kuzuia mmomonyoko wa udongo na kukauka kwa vyanzo hivyo vya maji;

xii. Sekta zinazohusika na usimamizi wa shughuli za umwagiliaji mashamba kuhakikisha matumizi sahihi ya maji yenye kuzingatia uhifadhi na ulinzi wa mazingira;

xiii. Taasisi za utafiti na vyuo vya elimu ya juu kufanya tafiti kuhusu kuzuia na kudhibiti kuenea kwa viumbe vamizi vinavyochangia uharibifu wa mazingira nchini;

xiv. Mamlaka zinazo husika na usimamizi wa hifadhi za wanyamapori kudhibiti matukio ya ajali za barabarani kwa wanyamapori; na

xv. Mamlaka zinazosimamia hifadhi za wanyamapori pamoja na mamlaka nyingine kuhakikisha zinadhibiti shughuli za binadamu pamoja na uvamizi katika maeneo ya mapito ya wanyamapori (shoroba) ili kupunguza uharibifu wa mazao, mali na binadamu kupoteza maisha kutokana na kuwepo mwingiliano wa wanyama na binadamu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt Selemani Jafo akiwa kwenye picha ya pamoja na Baadhi ya watumishi wa NEMC katika uzinduzi wa Maadhimisho ya siku ya Mazingira Duniani Iyumbu Dodoma.

# TUNAPOADHIMISHA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI TUJITAFAKARI KUHUSU UTUNZAJI WA MAZINGIRA - MHE. JOKATE MWEGELO



*Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe. Jokate Mwegelo akishiriki kilele cha Siku ya Mazingira Duniani ambayo kwa Mkoa wa Dar es Salaam yalifanyika Wilaya ya Temeke kwenye viwanja vya Zakhem Mbagala.*

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Wilaya ya Temeke Mhe Jokate Mwegelo alipokuwa mgeni rasmi katika sherehe za kilele cha maadhimisho ya siku ya mazingira duniani kilichofanyika katika viwanja vya Zakhem Mbagala jijini Dar es salaam.

Amesema uhifadhi na utunzaji wa mazingira ni suala linalotakiwa kuwekewa msisitizo katika utunzaji na uhifadhi wake kwani yakitunzwa vema yanapendeza na kuleta uhai kwa maisha ya wanadamu na viumbe hai, hivyo ni lazima kila Mtanzania ajitafakari kuhusu kutunza na kuhifadhi mazingira.

***"Tuepuke kuishi kwa mazoea hasa kwenye shughuli zetu za kila siku tusitupe taka hovyo. Unapokuwa na taka weka sehemu sahihi ya kutupia."*** Alisema Mhe. Jokate.

Ameongeza kuwa takwimu zinaonesha Tanzania inapoteza takribani hekta laki nne za misitu kwa mwaka, kutokana na ukataji wa miti kwa ajili ya matumizi mbalimbali hivyo ni lazima ifike muda wa kutumia nishati mbadala ili kuepuka mabadiliko ya Tabianchi.

Kwa upande wake Meneja wa Kanda ya Mashariki Kaskazini NEMC Bw. Arnold Mapinduzi amesema Sheria ya mazingira inasema kila mtu anayo haki ya kuishi katika mazingira safi na salama lakini imefafanua kuwa kila mtu anawajibu wa kutunza mazingira.

Bw. Mapinduzi pia amewasihi wananchi kutoa taarifa za uchafuzi wa Mazingira kwa Baraza la Taifa la hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC kwa namba za bure ambazo ni 0800110116 pindi wanapoona kuna uharibifu wa mazingira na namba hizi zinapokelewa kwa masaa 24.



*Watumishi wa NEMC wakiwa na washiriki wengine kwenye maadhimisho ya kilele cha Siku ya Mazingira Duniani yaliyofanyika kwenye viwanja vya Zakhem Mbagala Jijini Dar es Salaam.*

# NEMC KANDA YA MAGHARIBI YASHIRIKI MAONESHO YA KIMATAIFA YA BIASHARA



*Meneja Kanda ya Magharibi (katikati) Bw. Benjamin Dotto na Afisa Mazingira Bi. Edith Makungu wakitoa Elimu ya mazingira kwenye banda la NEMC kwenye maonesho ya Kimataifa ya biashara yaliyofanyika katika viwanja vya BOT Mkoani Kigoma.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) Kanda ya Magharibi, limeshiriki katika maonesho ya Kimataifa ya Biashara ya Nchi zinazozunguka ziwa Tanganyika, hafla iliiyofanyika katika viwanja vya BOT karibu na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Kigoma.

Akiongea katika maonesho hayo, Meneja wa NEMC Kanda ya Magharibi Bw. Benjamin Dotto amesema, NEMC imeshiriki ili kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusiana na masuala mbalimbali yakiwemo utunzaji na uhifadhi wa mazingira, usajili wa miradi, tathimini ya athari kwa mazingira Pamoja na ulipaji wa ada na tozo kwa wananchi.

“Maonesho haya ni muhimu yatasaidia sisi Baraza kutoa elimu kuhusiana na utunzaji na uhifadhi wa mazingira kwa wananchi wanaoshiriki katika maonesho haya ambayo yanajumuisha Nchi zote zinazozunguka Ziwa Tanganyika yani Tanzania, Rwanda, Burundi, Zambia na Congo DRC.” alisema Bwana Dotto

Naye Afisa Mazingira kutoka NEMC Kanda ya Mashariki Bi Edith Makungu alipokuwa akizungumza, amewataka wananchi kutilia mkazo suala zima la ulipaji wa ada na tozo za mazingira kwa wakati ikiwa ni pamoja na kushiriki katika maonesho yatakayowasaidia kupata elimu juu ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira.

***“Tunawasisitiza na kuwakumbusha wale wote ambao hawajalipa tozo na ada za mazingira kujitahidi kulipa ndani ya muda kwani kulipa ada na tozo za mazingira ni muhimu kwa mustakabali wa mendeleo ya Taifa letu”*** alisema.



*Meneja Mahusiano na Mawasiliano kwa Umma Bi. Irene John kutoka kushoto akitoa elimu ya mazingira kwenye banda la NEMC kwenye maonesho ya Kimataifa ya biashara yaliyofanyika katika viwanja vya BOT Mkoani Kigoma.*

# MHE. JAFO ATEMBELEA GHALA LA KUHIFADHIA NGOZI GHAFI TEMEKE




*Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Seleman Jafo akiwa kwenye kiwanda cha kuhifadhia ngozi ghafi kinachodaiwa kutoa harufu mbaya kwa wakazi naoishi karibu na ghala hilo lililopo Kurasini Jijini Dar es Salaam.*

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Seleman Jafo amefanya ziara ya ukaguzi wa mazingira katika ghala la kuhifadhi ngozi ghafi lililopo Kurasini Temeke jijini Dar es salaam.

Ziara hiyo imekuja mara baada ya Waziri Jafo kupokea malalamiko ya kuwepo kwa ghala linalohifadhi ngozi ghafi karibu na makazi ya watu hali inayosababisha kusambaa kwa harufu kali na kupelekea watu kushindwa kukaa ndani ya nyumba zao.

"Eneo kama hili lingeweza kuhifadhiwa bidhaa zingine kama mbao, saruji, nondo na bidhaa zingine ambazo zingeweza kuwa Rafiki kwa mazingira haya kwa sababu eneo hili lipo ndani ya makazi ya watu, ili kuepuka changamoto za uharibifu na uchafuzi wa mazingira ni lazima utaratibu wa kupata cheti cha mazingira kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ufuatwe". Amesema Mhe. Dkt Jafo

Aidha Mhe Jafo amemtaka mmiliki wa ghala hilo Bw. Shiri Mwandu kusitisha mara moja uingizaji wa ngozi nyingine katika ghala hilo ili kunusuru maisha ya wakazi wake ikiwa ni pamoja na kuepuka harufu mbaya inayoweza kusambaa na kusababisha kadhia kwa wananchi.

Katika hatua nyingine Mhe Jafo amefurahishwa na uanzishwaji wa kiwanda cha kuchakata na kurejeleza chupa za plastiki za rangi cha A-One kilichopo Mbagala hali inayopunguza uchafuzi wa mazingira unaosababishwa na chupa hizo.

"Nimefurahishwa sana Kwa kuanzishwa Kwa kiwanda hiki na leo nimefika ili kuona jinsi kinavyofanya kazi na nimefurahishwa sana, niwaombe muongeze vituo vya ukusanyaji wa chupa hizi Kwa Tanzania nzima ili nchi yetu iendelee kuwa safi na salama ".

Naye Afisa Afya na usalama wa kiwanda hicho Bw.Aurus George ameahidi kutekeleza agizo lililotolewa na Mhe. Waziri la kuongeza wigo mpana wa vituo vya ukusanyaji wa chupa hali itakayokuza fursa kwa watanzania kufanya biashara na kutunza mazingira kwa wale watakaokuwa wanakusanya chupa hizo na kuziuza kwao.

Kwa upande wake mwekezaji wa kiwanda hicho Bw. Prashant Plaint amesema anampango wa kuongeza nguvu zaidi katika uzalishaji na kwa mwaka ujao 2023 anatarajia kurejeleza chupa mara mbili zaidi ya sasa.



*Sehemu ya ngozi ghafi zinazodaiwa na kutoa harufu mbaya zikiwa zimehifadhiwa kwenye ghala la kuhifadhia ngozi lililopo Kurasini Jijini Dar es Salaam.*

# UMUHIMU WA UPANDAJI MITI KATIKA KUKABILIANA NA MABADILIKO YA TABIANCHI

Mabadiliko ya tabianchi ni miongoni mwa changamoto kubwa zinazoikumba Dunia kutokana na shughuli za kibinadamu. Athari ya mabadiliko ya tabianchi kama vile ongezeko la joto duniani, kupungua kwa kiwango cha mvua, mabadiliko ya utaratibu wa mvua na kupanda kwa kiwango cha maji baharini ni athari kwa maisha ya binadamu kiuchumi na kijamii. Juhudi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi zimewekwa ili kukabiliana ongezeko la athari za mazingira na hivyo nchi zote duniani kuchukua hatua za kutunza na kulinda mazingira.

Katika kuhakikisha juhudi za kutunza mazingira yetu zinatiliwa mkazo, nchi mbalimbali zinafuata Sera na Kanuni za Mazingira ili kupunguza na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, kwa kushirikiana na wananchi, Serikali ya Tanzania imeweka mipango na mikakati mbalimbali ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Kutunza misitu pamoja na kupanda miti ni moja kati ya hatua muhimu zinazochukuliwa ili kuhakikisha ulinzi na ustawi wa mazingira kwa kizazi cha sasa na cha baadae. Juhudi hizi zimekua na mafanikio kiasi ikilinganisha na athari kubwa zinazosababishwa na shughuli za kibinadamu zikihusisha ukatajia hovyo wa miti kwa ajili ya mbao, kuni na mkaa.

Hatua mbalimbali za kuzuia ukataji miti zimechukuliwa kwa kuanzishwa kwa kampeni za kuhamasisha upandaji miti katika maeneo mbalimbali, kama vile "KATA MTI PANDA MITI". Pamoja na kauli mbiu ya hivi karibuni iliyoanzishwa na Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Mhe. Dkt. Selemani Jafo ijulikanayo kama "SOMA NA MTI", inahamasisha upandaji wa miti katika taasisi muhimu kama mashuleni, vyuo, magereza pamoja na taasisi mbalimbali.

Aidha, kuhamasisha matumizi ya nishati mbadala kama vile gesi, majiko banifu na mkaa unaotengenezwa kwa makaratasi kwa matumizi mbalimbali ya binadamu kama vile kupikia na kadhalika, yamekuwa muhimu ili kupunguza ukataji wa miti na uharibifu wa misitu kwa kiwango kikubwa. Pia, ukataji wa miti kwa ajili ya kuni na mkaa huchangia kwa kiasi kikubwa kuondoa mfumo ambao kusaidia kutunza hewa ya ukaa. Tafiti mbalimbali zinaonyesha ongezeko kubwa la uzalishaji wa hewa ya ukaa huchangia kwa kiasi kikubwa kuongezeka kwa joto duniani. Hewa hii inazalishwa na shughuli za maendeleo kama vile viwanda vinavyotoa gesi chafu inayosambaa angani, moshi wa magari na shughuli nyingine zinazochangia uharibifu wa mazingira. Hewa hii inapokuwa kwenye anga inakuwa ni eneo la kuhifadhi joto linalotokana na miale ya jua na kusababisha kuongezeka kwa joto duniani.

Mbali na hilo kampeni hizi zimetilia mkazo utunzaji wa ardhi oevu ambayo ni muhimu kwa ikolojia. Utunzaji sahihi wa maeneo oevu ni moja ya nyenzo muhimu za ustawi wa mazingira na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Maeneo oevu husaidia kufyonza hewa ya ukaa, kutunza maji kwa ajili ya kuzuia mafuriko, kuchuja sumu na uchafu pamoja na kusaidia kupatikana kwa maji kwa misimu yote. Hivyo ni muhimu kuyatunza maeneo haya ili kuepusha majanga ya kimazingira kama vile ukame na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Jitihada zinazofanywa na serikali ni pamoja na matumizi ya njia bora na za kisasa kwenye kilimo ili kukabiliana na atahri za mabadiliko ya tabia nchi. Serikali kupitia wadau mbalimbali wa mazingira inahamasisha matumizi ya njia bora za kilimo kama umwagiliaji na kutokutegemea mvua pekee, kuhimiza kutokuchoma moto mashamba katika uandaaji wa mashamba kwa ajili ya kilimo na kulima kwa kutumia matuta hasa sehemu za miteremko.

Vilevile, mikakati inafanywa na wataalamu wa mazingira kuhusiana na matumizi ya njia bora za kilimo zisizo athiri uoto wa asili na rutuba ya udongo. Hii inasaidia kuepusha janga la ukame, uharibifu wa mazingira na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi.

Sambamba na hayo, elimu inapaswa kuendelea kutolewa kwa jamii kuhusu madhara ya uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kuhimiza njia bora na sahihi za kutunza mazingira ikiwemo upandaji wa miti, njia bora za kilimo, matumizi ya nishati mbadala na hivyo kusaidia kuongoa mfumo ikolojia.



*Athari ya mabadiliko ya tabianchi katika mazingira.*

# NEMC YATOA VIFAA NA KUSHIRIKI ZOEZI LA USAFI - KISUTU



Meneja Uhusiano na Mawasiliano kwa Umma kutoka NEMC Bi. Irene John akikabidhi vifaa vya usafi kwa kampuni ya Orbit Media kwa ajili ya shughuli za usafi wa mazingira kwenye mtaa wa Kisutu Jijini Dar es Salaam.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeunga mkono juhudi za Serikali katika kutunza mazingira kwa kushiriki katika zoezi la usafi kwenye baadhi ya maeneo ya mtaa wa Kisutu pamoja na kutoa vifaa vya kufanyia usafi kama fagio,vikinga mikono na barakoa kwa Kampuni ya Orbit Media inayoshirikiana na serikali ya mtaa wa Kisutu jijini Dar es salaam ili kuwezesha wananchi kutunza mazingira.

Akikabidhi vifaa hivyo vya usafi kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira, Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma Bi. Irene John amesema " Tumefurahi leo kuungana na wenzetu mahali hapa kufanya usafi kwa sababu ni jukumu letu kuhakikisha kuwa mazingira yanakuwa safi na salama. Maana jiji letu likiwa safi hakutakuwa na magonjwa kama kipindupindu na miili yetu itakua na afya njema na kuongeza nguvu kazi ya Taifa katika kukuza uchumi. Hivyo NEMC inatoa wito kwa taasisi nyingine wajitoe katika kuunga mkono juhudi za Serikali za kuhakikisha kuwa Miji na Majiji yanakuwa safi na salama."

Naye Mwenyekiti wa Serikali ya mtaa wa Kisutu Bi. Mariam Bawaziri ameishukuru NEMC kwa kutoa vifaa pamoja na kushiriki zoezi la kufanya usafi katika baadhi ya maeneo ya mtaa wa Kisutu ikiwa ni moja ya jitihada za kuunga mkono juhudi za Rais Samia Suluhu Hassan na Mkuu wa Mkoa kwa kuhakikisha kuwa jiji linakuwa safi.

Aidha Mkurugenzi wa kampuni ya Orbit Media Bw. Moses Mwakibolwa ametoa shukrani kwa NEMC baada ya kupokea vifaa vilivyotolewa kwa ajili ya zoezi la usafi wa jiji. Pia ameishukuru Serikali ya mtaa wa Kisutu pamoja na wadau waliojitokeza kufanya usafi na kutoa pongezi kwa Serikali na Mkuu wa Mkoa wa Dar es salaam kwa kuhimizia usafi kwa kuwa Dar es Salaam ni kitovu cha biashara.

Kwa upande wake mmoja wa wanachi wa mtaa wa Kisutu Bw. Leonce Safari ameishukuru NEMC kwa kutoa vifaa na kushiriki zoezi la usafi katika mtaa wa Kisutu na kuishukuru Serikali kwa ajili ya kubuni zoezi hilo na kuahidi kuvitumia vifaa hivyo katika kutekeleza kampeni ya kuweka jiji safi.



Watumishi kutoka NEMC wakiwa kwenye picha ya pamoja na wafanyakazi wa Orbit Media mara baada ya kukabidhiwa vifaa kwa ajili ya usafi na utunzaji wa mazingira kwenye mtaa wa Kisutu Jijini Dar es Salaam.

# NEMC YASHIRIKI ZOEZI LA KUFANYA USAFI KATIKA FUKWE ZA RAINBOW KAWE -JIJINI DAR ES SALAAM



*Wadau mbalimbali wa mazingira wakishiriki zoezi la kufanya usafi katika fukwe za Rainbow, Kawe jijini Dar es salaam na kushiriki pia mjadala mfupi kuhusu mazingira.*

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeshiriki katika zoezi la kufanya usafi katika fukwe za Rainbow zilizopo Kawe jijini Dar es salaam .Tukio hilo limeandaliwa na kuratibiwa na asasi za mazingira ambazo ni Sustainable Development Network SND pamoja na Human Dignity and Environment Care Organization HUDEFO lengo ikiwa ni kuweka mazingira safi na salama.

Akizungumzia kuhusu zoezi hilo mwenyekiti wa asasi isiyo ya kiserikali ya Sustainable Development Network (SDN) Fred Kwezi amesema huu ni mwendelezo wa siku 30 za kusafisha mazingira na ambapo ndani yake kulikuwa na kampeni ya kuirejesha fukwe ya Rainbow ambayo tayari ilikuwa imepoteza uzuri wake kutokana na uchafu ulikokuwa umekithiri katika fukwe hiyo. " Hapa unavyopaona Leo hii ni jitihada zetu, palikuwa hapatazamiki na sasa pameanza kuvutia bila shaka shughuli za utalii zitarejea katika fukwe hizi".

Kwa upande wake mkurugenzi wa asasi isiyo kuwa ya kiserikali ya Human Dignity and Environmental Care Organization (HUDEFO) Bi. Sarah Pima amesema jamii inapaswa kuelewa ya kuwa mazingira ni kila kitu, hivyo kila mmoja wetu ashiriki kulinda mazingira kuanzia nyumbani mpaka kwenye jamii yote kwa ujumla. Ameongeza kuwa fukwe kama hiyo inaweza kuiingizia Serikali pato pale ambapo watalii watafika kwa ajili ya kutalii na kujionea mandhari nzuri ya fukwe hiyo hivyo mazingira yakiwa machafu watalii hawawezi kuja Kwa sababu uchafu hauvutii .

Naye Meneja wa Kanda ya Mashariki Kaskazini kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC Bw. Anold Mapinduzi amesema amefurahishwa sana kuona asasi na wanajamii kwa ujumla wako mstari wa mbele katika kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa na kulindwa Kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Bw. Mapinduzi pia amesema katika kuelekea kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Dunia hapo ambayo kitaifa yanafanyika Mkoani Dodoma NEMC ikiwa ni wasimamizi wa utekelezaji wa Sheria ya Mazingira wako tayari kuungana na wadau wote wa Mazingira ili kuhakikisha watu wote pamoja na viumbe hai wengine wanaishi katika mazingira safi na salama.




*Baadhi ya wadau a Mazingira wakishiriki zoezi la kufanya usafi katika fukwe za Rainbow Kawe jijini Dar es salaam mapema Leo asubuhi tarehe 4/06/2022. Zoezi hilo limeratibiwa na asasi za mazingira (Sustanable Development Network (SND) na Human Dignity and Environmental Care Organization ( HUDEFO).*

*Meneja wa Kanda ya Mashariki Kaskazini kutoka Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira NEMC Bw. Anold Mapinduzi akishiriki kikamilifu zoezi la kufanya usafi katika fukwe za Rainbow ilizopo Kawe jijini Dar es salaam mapema Leo asubuhi.*





*Baadhi ya watumishi wa NEMC wakishiriki zoezi la kufanya usafi katika fukwe za Rainbow zilizopo Kawe jijini Dar es salaam.*

# GEREJI BUBU NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA NA AFYA YA JAMII



Pamoja na umuhimu wake kwa kuimarisha matumizi ya vifaa, gereji zimetajwa kuwa na atahri hasi za mazingira. Aidha, gereji zimekuwa ni eneo ambalo limelalamikiwa kusababisha kelele, uzagaaji wa taka ngumu pamoja na uchafuzi wa mazingira kutokana na mafuta machafu (waste oil). Mafuta haya yanakuwa yametumika na kupoteza asili yake iliyokuwa awali kabla ya kutumika. Tutambue kuwa kuna vyanzo vingi vya upatikanaji wa mafuta machafu ikiwemo gereji za magari na pikipiki, mitambo ya viwandani, taka tope (sludge) la matanki ya meli, vituo vya kuuzia mafuta n.k.

Mafuta machafu ni aina moja wapo ya taka hatarishi kwa mujibu wa Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 na Kanuni mpya za Usimamizi wa Taka Hatarishi za mwaka 2021 [The Environmental Management (Hazardous Waste Control and Management) Regulations, 2021]. Kanuni hii inamuelekeza kila mtu anayetaka kujihusisha na usafirishaji, ukusanyaji na urejerezaji wa taka hatarishi kuzingatia Sheria hiyo na kupat vibali husika.

Gereji ni moja ya chanzo cha uzalishaji wa mafuta machafu (waste oil) katika maeneo mengi hapa nchini. Pia kumekuwa na malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya umwagaji hovyo wa mafuta machafu hasa katika gereji bubu zilizopo kwenye makazi ya watu. Tunaposema gereji bubu tuna maana kuwa ni gereji ambazo hazijasajiliwa na zinafanya shughuli zake bila ya kuzingatia Sheria na kupelekea athari kubwa kwa mazingira na binadamu.

Gereji bubu zinachangia kwa kiasi kikubwa kwenye umwagaji wa mafuta machafu hovyo yanayotoka kwenye magari na pikipiki bila ya kufuata utaratibu uliowekwa. Hali hii husababisha uchafuzi wa mazingira nchini. Na sifa ya mafuta ni kusambaa kwenye eno kubwa. Tunaposema mazingira ni kila kitu kinacho tuzunguka maana yake ni kuwa tunapofanya uharibifu sehemu moja kwa namna moja au nyingine tunasababisha madhara sehemu nyingine bila kujua.

Tukumbuke kuwa shughuli za gereji zinachangia kwa kiasi kikubwa kwenye kipato cha mwananchi na kumuwezesha kujikimu kimaisha. Shughuli zote hizi zinatakiwa zifanyike kwa kuzingatia miongozo ya uhifadhi wa mazingira. Kwa maana hiyo, ni wajibu wa kila mwananchi kufanya kazi zake kwa kuzingatia Sheria na Kanuni ya Mazingira. Kuna fursa nyingi ztokanazo na matumizi ya mafuta machafu ikiwemo kurejeleza na kutumika (recycling) lakini pia yanaweza kutumika tena kwa matumizi mengine (reuse). Hivyo, mhusika yeyote anayetaka kutumia fursa hizo inalazimu kuomba kibali NEMC ili kuhakikisha shughuli hizo zinafanyika pasipo kuharibu mazingira.

Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) ni msimamizi mkuu wa Mazingira nchini Tanzania. Kutokana na mamlaka hayo, Baraza wametembelea na kukagua maeneo kadhaa ya gereji, viwanda na vituo vya mafuta katika mikoa mbalimbali na kujionea hali halisi ya mazingira. NEMC imekuwa ikipokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya uwepo wa gereji bubu ambazo zinafanya shughuli zake bila ya kuzingatia sheria na zimekuwa kero katika makazi mengi ya watu.

Mkazi mmoja, wa maeneo ya Mpakani Mbagala Zakheem jijini Dar es Salaam ameeleza kuwa uwepo wa gereji bubu katika makazi yao umekuwa kero kubwa hususan katika suala zima la umwagaji mafuta machafu kwenye mazingira. Hali hii imepelekea watu kuvuta hewa chafu ambayo inaathiri afya zao. Mkazi huyo ameiomba serikali kufuatilia malalamiko hayo na kuwatengea maeneo maalumu wale wote wanaojishughulisha na gereji ili kuepuka kadhia hizo. Mkazi huyo amesema kuwa gereji hizo zinafanywa na vijana na kunakuwa na kelele nyingi ambazo zinasababisha kukosa usingizi wanapotaka kupumzika na baadaye kuathiri afya zao.

Mkurugenzi Mkuu wa NEMC Mhandisi Dkt. Samuel G. Mafwenga amesema kuwa sheria ya mazingira iheshimiwe kwani sheria hii inamtaka kila mtu kutunza na kuhifadhi mazingira kwa kizazi kilichopo na kijacho. Amesema kuwa kila mwekezaji anapotaka kutekeleza mradi anatakiwa kujua kuwa Wizara ya Ardhi imeweka kitu kinachoitwa mipango miji ambayo inaainisha kila shughuli inafanyika katika eneo lipi kwa kuzingatia maeneo ya makazi, viwanda, shule, hospital na nyumba za ibada hii ni kutokana na kuepusha usumbufu, migogoro na uharibifu wa mazingira.

Dkt. Mafwenga alisisitiza kuwa kuwa shughuli zote zikifanyika kwa utaratibu hakutakuwa na malalamiko wala migogoro. Wawekezaji wengi wanasababisha migogoro kutokana na kuvunja Sheria na taratibu zilizowekwa na kama watakuwa wanafuata Sheria basi hakutakuwa na malalamiko wala uharibifu wa mazingira katika nchi yetu alifafanua Mkurugenzi Mkuu.

Umwagaji wa mafuta machafu una athari nyingi kimazingira na afya kwa binadamu. Binadamu anaweza kuathirika kupitia kuvuta hewa, kumeza au kugusa, japo pia anaweza kuathirika na madini tembo yanayopatikana katika mafuta machafu kama vile madini ya risasi (lead) na kusababisha magonjwa ya saratani. Kimazingira mafuta machafu yanapomwagika chini yanaharibu mazingira pale yanapoingia kwenye mchanga/udongo yanaenda kuchanganyika na maji yaliyo chini ya ardhi (visima) na pengine hutiririka na kuingia kwenye vyanzo vya maji ambavyo binadamu huvitegemea kwa kupata maji ya kunywa na kutumia kwa matumizi mengine kama kilimo n.k

Umwagaji wa mafuta machafu katika ardhi huathiri mimea na viumbe vingine ambavyo havionekani kwa macho ambapo viumbe hawa ni muhimu kwenye mfumo mzima wa ikolojia. Hivyo kila mtu anawajibu wa kuzingatia Sheria ya mazingira ili kulinda mazingira na viumbe vinavyotuzunguka. Ukizingatia maelekezo ya wataalamu utachangia kulinda na kutunza mazingira kwa faida ya taifa zima.

# VIWANDA ENDELEVU, UCHUMI IMARA KWA MAZINGIRA SAFI NA SALAMA





Sekta ya viwanda ni moja kati ya sekta muhimu katika ukuaji wa uchumi wa nchi na inapewa kipaumbele katika mpango wa Taifa wa kukuza uchumi. Viwanda nchini Tanzania ni miongoni mwa sekta kubwa inayoongeza pato la Taifa, na sekta hii ni muhimu sana kwani inatoa ajira kwa vijana na kupelekea uchumi wa nchi kukua kwa kasi kubwa. Sekta hii imekuwa kutokana na uanzishwaji wa viwanda vingi vikubwa vya kati na vile vidogo vidogo. Kwa mfano viwanda vya nguo, ngozi, saruji, uchakataji wa chuma na plastiki.

Viwanda vinachochea mageuzi ya kimfumo kwenye jamii katika kilimo na madini. Kuwa na viwanda vingi nchini kunachangia uwepo wa bidhaa ndani ya nchi na kupanua wigo wa upatikanaji wa bidhaa hizo. Hali hii inaongeza wigo wa uchaguzi katika kukidhi mahitaji ya watu.

Ukuaji wa shughuli za viwanda kunategemeana na sekta nyingine. Kwa mfano, kilimo ni moja ya sekta inayochangia ka kiasi kikubwa katika ukuaji ukuaji wa viwanda nchini kwani malighafi nyingi zinazotumika viwandani zinatokana na kilimo. Hivyo, kilimo ni chachu ya kuwepo kwa viwanda na huchochea wananchi kuhamasika kulima ili kuuza malighafi zao katika viwanda vilivyopo nchini.

Uchumi wa Nchi pia hutegemea uwepo wa viwanda kwa kutoa ajira kwa wananchi na ushuru kwa ajili ya maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Kwa mfano, kilimo cha pamba kinachochea viwanda kupata malighafi kwa ajili ya kutengeneza nguo, inachangia uwepo wa ajira kwa wananchi wanaojihusisha na kilimo pamoja na uzalishaji viwandani. Hivyo hatuwezi kutenganisha viwanda na kilimo.

Viwanda vinachangia uchumi wa nchi kukua na kukuza uchumi wa mwananchi mmojammoja na kukidhi mahitaji yao. Licha ya faida nyingi zitokanazo na kukua kwa viwanda nchini, ikumbukwe pia kuwa viwanda vina mchango mkubwa kwenye suala zima la athari za mazingira.

Uharibifu wa mazingira utokanao na shughuli za viwanda umegawanyika katika makundi kadhaa. Uharibifu wa mazingira unaweza kuelezewa kwa kuzingatia aina ya bidhaa zinazozalishwa, eneo ambapo uzalishaji unafanyika au mifumo inayotumika ya uzalishaji. Kuna baadhi ya aina za viwanda ambavyo huzalisha taka sumu ambazo ni chanzo kikubwa cha uchafuzi na uharibifu wa mazingira. Tatizo la uchafuzi wa mazingira hususan kwa wenye viwanda husababishwa matumizi ya teknolojia duni na zisizo salama kwa mazingira, uelewa mdogo wa sheria na wenye viwanda kutokuona umuhimu hifadhi ya mazingira.

Uzoefu uliobainishwa na Baraza ni kwa viwanda vingi kuwa na changamoto nyingi za mazingira hali ambayo husababishwa na wamiliki wa viwanda kutokuzingatia Sheria ya Mazingira. Aidha, athari nyingi za kimazingira katika viwanda hutokana shughuli zenyewe za uzalishaji bidhaa kutokuzingatia mpango wa usimamizi na ufatiliaji wa mazingira (Environmental Management and Monitoring Plan) huandaliwa mapema wakati wa andiko la TAM (Tathimini ya Athari kwa Mazingira). Athari zingine zinazoendana na mazingira, ni athari za kijamii. Hivyo, ili kuweza kufikia lengo la kufanya uzalishaji ulio thabiti kwa kizazi kilichopo na kijacho ni muhimu kwa viwanda kuwa na mifumo thabiti ya uhifadhi wa mazingira.

Kuzingatia utunzaji wa mazingira ni jambo la msingi ili kuwa na uchumi endelevu wenye kuzingatia uhifadhi wa mazingira. Mazingira yakiharibika itakuwa ni vigumu kuwa na uchumi endelevu. Hivyo, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeendelea kuhakikisha mazingira yanakuwa safi na salama ili kuwezesha wananchi pamoja na wawekezaji kufanya shughuli zao kwa kuzingatia Sheria ya Mazingira ya Mwaka 2004 pamoja na Kanuni zake. Hii ni kulifanya Taifa kuwa na viwanda endelevu, uchumi imara na mazingira safi na salama kwa maendeleo ya nchi.

Licha ya kuwepo Sheria ya usimamizi wa Mazingira, uharibifu wa mazingira unaotokana na viwanda upo wa aina tofauti. Viwanda husalisha taka ngumu, majitaka, taka za sumu, na hewa chafu. Aidha, majitaka yaliyochanganyika na kemikali kutoka viwandani yanayotiririshwa kuelekea kwenye mazingira na vyanzo vya maji. Licha ya Baraza kuchukua hatua stahiki kwa viwanda visivyo zingatia taratibu za mazingira, bado kuna baadhi ya wenye viwanda kuendelea kuchafua mazingira.

Baraza limeendelea kufanya kaguzi kwenye viwanda ili kuhakikisha uzalishaji wa bidhaa katika viwanda hivyo unafanyika pasipo kuathiri mazingira. Changamoto za uchafuzi wa mazingira zipo nyingi na Baraza limeendelea kupokea malalamiko mengi kutoka kwa wananchi juu ya wamiliki wa viwanda kuwa na tabia ya kutiririsha maji taka kwenye mazingira pasipo kuwa wameyatibu Aidha, suala hili imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wanaoishi maeneo yanayozunguka kutokana na athari kiafya kutokana umwagaji ovyo wa majitaka hayo.

Licha ya jitihada nyingi zinazofanywa na Serikali za udhibiti wa uharibifu wa mazingira kwa kutoza faini na kusitisha shughuli zinazofanywa na viwanda, bado haijasaidia kupunguza tatizo husika.

MAKALA:



# IFAHAMU SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI TAREHE 5 JUNI KILA MWAKA

Tarehe 5 Juni ya kila mwaka Watanzania tunaungana na mataifa mengine ulimwenguni kuadhimisha Siku ya Mazingira Duniani. Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani yaliidhinishwa na Baraza la Umoja wa Mataifa la mwaka 1972, wakati wa mkutano wa kwanza wa Umoja wa Mataifa uliohusu Mazingira huko Stockholm, nchini Sweden.

Aidha, azimio la kuunda Shirika la Umoja wa Mataifa la kushughulikia Mazingira Duniani, yaani United Nations Environment Programme (UNEP) lilipitishwa siku hiyo. Tangu wakati huo, nchi mbalimbali duniani zimekuwa zikiadhimisha Siku ya Mazingira Duniani kila mwaka tarehe 5 Juni. Aidha, Jumuia ya Umoja wa Mataifa hutoa ujumbe ujumbe maalumu unotakiwa kuzingatiwa kila mwaka.

Tanzania pia imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha mazingira yanasimamiwa, yanahifadhiwa na kulindwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho. Kwa kipindi chote tangu kuundwa kwake, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) limeendelea kusimamia kikamilifu hifadhi za mazingira hap nchini. Jitihada zinazofanywa na Baraza ni pamoja na kuhakikisha linakuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha mazingira ni salama na kuwa afya ya jamii inalindwa. Katika utekelezaji wa majukumu yake, Baraza limebaini kuwepo kwa mwamko hafifu kwa wananchi katika suala zima la uhifadhi na usimamizi wa mazingira. Aidha, hali inayojitokeza ni kwa wananchi walio wengi kusibiri hadi ifikapo kipindi cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira duniani ndio watoke kujumuika na wengine kufanya usafi au shughuli zozote za uhifadhi na utunzaji wa mazingira tofauti na siku nyingine za kawaida.

Tunaamini kuwa suala la kutunza na kuhifadhi mazingira ni la kila mmoja wetu na Mazingira hayatunzwi siku moja. Ni lazima kuwepo na mwendelezo wa kila siku ili mazingira yaendelee kuwa salama afya ya jamii na kwa maendeleo endelevu. Hivyo watanzania wote hatuna budi kuwa na utamaduni wa kuhifadhi na kutunza mazingira pasipo kushurutishwa kwa kuwa mazingira ni uhai na tunategemea kupata kila kitu kutoka kwenye Mazingira yetu.

Waziri Mkuu Kassim Majaliwa Majaliwa (katikati) akikata utepe wakati wa akizindua Mpango Kabambe wa Uhifadhi wa Mazingira katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani iliyofanyika Kitaifa jijini Dodoma ambapo alikuwa mgeni rasmi. Na wa kwanza kulia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira Dkt. Selemani Jafo.

Madhumuni ya Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani ni kuhamasisha jamii duniani kote kuelewa masuala yahusuyo mazingira na pia kuhamasisha watu na jamii mbalimbali duniani kuwa mstari wa mbele katika kuchukua hatua kuhifadhi na kulinda mazingira. Aidha, tunatumia siku hii kutoa fursa kwa jamii kufahamu kwamba wana wajibu wa kudhibiti uharibifu wa mazingira ii kuzuia madhara na mabadiliko hasi kwa jamii na kufanya mazingira kuwa salama na safi katika maisha yetu na vizazi vyetu vya sasa na vijavyo.

Jamii inapaswa kufahamu ya kuwa Siku ya Mazingira Duniani ni jukwaa la Kimataifa la kuchochea msukumo na mabadiliko chanya na kutoa msukumo kwa jamii kutafakari upya kuhusu jinsi inavyoweza kutumia rasilimali dunia zinazoweza kuisha. Vilevile kuhamasisha mashirika ya biashara kubuni mifumo isiyochafua mazingira; wakulima na wazalishaji kuzalisha kwa njia endelevu; Serikali ziwekeze katika uboreshaji wa mazingira; walimu kushawishi wanafunzi kuchukua hatua za hifadhi ya mazingira, na vijana weledi na maarifa kwenye masuala ya mazingira. .

Hivyo, kila mmoja wetu duniani kote atambue ya kuwa jukumu la kuhifadhi na kutunza mazingira ni letu sote, tutaweza kuyaokoa mazingira kutoka kwenye hatari ya kuharibika na kupotea kwa viumbe ambao wanategemea mazingira na mifumo ikolojia. Kwa ujumla Dunia ni Moja Tu, Tunza Mazingira.





# UMUHIMU WA UPANDAJI MITI KWENYE UHIFADHI WA MAZINGIRA

Upandaji miti unamaanisha kupanda miti katika maeneo ambayo mwanzoni hayakuwa na miti au ambapo miti ilikatwa. Aidha, upandaji miti hufanywa kuboresha hali ya mazingira katika eneo husika. Vilevile, shughuli za upandaji ni uingizwaji wa misitu au misitu iliyopotea. Shughuli hii ni kubwa na muhimu inayohitaji kujua hali ya hewa, aina ya udongo wa eneo litakalopandwa miti ikiambatana na upatikana wa maji katika eneo hilo. Ni muhimu pia kuelewa mahitaji ya kibaiolojia ya aina ya miti (specie) itakayopandwa. Miti inastawi vizuri iwapo imepandwa katika eneo ambalo mazingira yanalingana na mahitaji ya aina ya miti husika. Kwa hivyo ni vyema wakati wa kuchagua miti ya kupanda kuoanisha aina ya miti na mazingira yanayofaa hii ikiwa ni pamoja na sifa za udongo na kiwango cha unyevu. Aidha zoezi hili litakuwa timilifu iwapo taasisi zinazojihusisha na tafiti za misitu (Tanzania Forestry Research Institute - TAFORI) zitakuwa zimeshirikishwa kikamilifu kwenye zoezi husika

Miti inayotakiwa kupandwa hapa nchini ni ya aina nyingi, ikiwepo ya asili na ya kigeni. Nchi ya Tanzania ni kubwa yenye maeneo yanayotofautiana katika aina, rutuba na kina cha udongo, kiasi cha nyongo (base) au tindikali (acid) katika udongo, hali ya hewa (kiasi cha mvua na nyuzi joto), mwinuko kutoka usawa wa bahari, umbali kutoka ufukwe wa bahari, mteremko au tambarare n.k. Kwa mantiki hiyo, kuna haja ya kuangalia mwongozo katika zoezi la kuoanisha aina ya miti na mahali panapofaa kuipanda. Aidha, madhumuni ya kupanda miti sharti yajulikane kabla ya kupanda, kuchagua aina ya miti ya kupanda. Umbali kati ya mti na mti itategemea matumizi yanayokusudiwa wakati miti itakapovunwa. Madhumuni yanaweza yakawa ni kupata nishati (kuni, mkaa au vyote), mbao, nguzo, kivuli, mapambo, matunda, dawa, kurutubisha ardhi, kuzuia mmomonyoko wa udongo n.k.

Mbinu za upandaji miti ni tofauti na hutofautiana kulingana na aina mahususi za upandaji wa miti na mahitaji ya spishi zitakazopandwa. Aidha, kwa ujumla, ni muhimu kujifunza hali ya hewa, aina ya udongo na upatikanaji wa maji katika eneo husika. Shimo la kupanda miche ya miti liwe na upana na urefu unaokubalika kutokana na sifa za aina yam mmea/mti husika. Wakati wa upandaji, udongo unatakiwa kushindiliwa vizuri ili kuwezesha mizizi kushikamana vizuri na udongo. Vilevile, ili miche mingi iliyopandwa iweze kupona na kustawi vyema, inabidi kuzingatia yafutayo:

1. Kuoanisha aina ya miti na mahali pa kupanda
2. Kutayarisha au kutifua ardhi vizuri ili kusaidia mizizi kupenya kwa urahisi na kunyonya virutubisho;
3. Kudhibiti magugu;
4. Kuchimba mashimo yenye kina na upana unaostahili;
5. Kuacha nafasi inayostahili kati ya mti na mti; na
6. Kuweka mbolea pale inapostahili.



Miti ina matumizi mengi na baadhi ya matumizi ya miti ni kama vile: mbao, nguzo, chakula cha binadamu na mifugo, kuni, mkaa, madawa, hifadhi ya vyanzo vya maji, kurutubisha na kuzuia mmomonyoko wa udongo, kuboresha hali ya hewa, mapambo, n.k. Mbali na kuwa na faida nyingi ikiwemo kulinda vyanzo vya maji, kuvuta mvua, kuwa makazi ya viumbe hai mbalimbali, kutoa nishati ya kuni na mkaa na kutoa mbao, miti pia husaidia kufyonza na kuhifadhi hewa ukaa inayozalishwa na binadamu kutokana na shughuli mbalimbali. Ambapo madhara yanayotokana na hewa ukaa ni pamoja na kuharibu blanketi la ozoni na kusababisha miale mikali ya jua kuufikia uso wa dunia, hali inayosababisha ongezeko la joto na maradhi ya saratani ya ngozi.

Kutokana na hayo, kumekuwepo na kampeni mbalimbali zilishorikisha na viongozi mbalimbali wa kitaifa zikiwa na lengo kuu la kufanya mazingira kuwa safi na salama kwa binadamu. Kampeni kama (1) Tanzania ya Kijani inawezekana- iliyokuwa na lengo la kujenga upya nchi ya kijani na kupunguza atahri zinazosababishwa na mabadiliko ya hali ya hewa. (2) Pendezesha Tanzania- iliyokuwa na lengo la kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. (3) Kata mti panda mti- iliyokuwa na lengo la kuzuia ukataji wa miti hovyo kwenye misitu ya hifadhi. (4) Soma na mti- ambayo inamtaka kila mwanafunzi nchini Tanzania apande mti na kuutunza mpaka pale atakapokuwa anahitimu masomo yake. Kampeni zote hizi na nyinginezo zina madhumuni ya kupanda na mabadiliko ya tabianchi yenye madhara mengi kwa binadamu na viumbe hai.

Mpango huu wa upandaji miti umelenga kuongeza jitihada za kuhifadhi mazingira pamoja na kudhibiti hewa ya ukaa na hivyo kupunguza ongezeko la joto duniani na athari za mabadiliko ya tabianchi. Hivyo basi, tupande miti kwani maisha yetu yanategemea sana miti sababu Miti ni Uhai. Tunatakiwa kupanda miti na kuitunza ili ituletee faida, Tanzania ni moja Tu, Tunza Mazingira.

# MADHARA YA MAFUTA NA MAFUTA MACHAFU KATIKA MAZINGIRA

Mafuta au mafuta machafu ni kemikali inayojumuisha vitu vya Haidrojeni na Kaboni ikiwa ni pamoja na bidhaa za petrol, mafuta ya wanyama, mafuta ya mboga na mengine. Kwa ujumla mafuta machafu yana madhara katika afya na mazingira kwani yanapoingia katika mazingira haswa kwenye vyanzo vya maji, hubadilisha Ikolojia ya eneo kwa kuathiri mlolongo wa chakula ambao viumbe wa majini hutegemea, kupunguza oksijeni kwenye maji japo ukubwa wa madhara hutegemea sifa ya mafuta yenyewe. Mafuta machafu yanaweza kuwa na viashiria vya sumu ndani yake ambayo yana uwezo wa kuuwa moja kwa moja viumbe na mimea katika mazingira.

Kwa Mtanzania wa kawaida mafuta kumwagika ni pamoja na matukio ya kuvuja au kupasuka kwa matanki ya kuhifadhi mafuta na pia mabomba ya kusafirisha mafuta. Halii hii inapojitokeza husababisha majanga makubwa ikiwa ni pamoja na uchafuzi wa mazingira, athari kwa afya ya jamii na hata kupelekea vifo kwa binadamu na viumbe wengine. Hata kwenye maeneo ya ya jamii zetu huwa tunaona mafuta au mafuta machafu yakiwa yamemwagika katika ardhi au yakielea katika mikondo ya maji. Hali hii pia hujitokeza kwenye gereji na maeneo ya kuoshea magari ambapo mafuta humwagwa bila utaratibu.

Ni muhimu kukumbuka kuwa mafuta yakimwagika ardhini hatima yake ni kwenye mikondo ya maji na kuingia katika maziwa, mito, na ardhi oevu ambapo husababisha madhara kwa afya za jamii, viumbe na mazingira kwa ujumla. Mafuta au mafuta machafu yanapomwagika katika mazingira na kufikia vyanzo vya maji yanaweza kudhuru viumbe wanaoishi na kutegemea maji hayo.

Mazingira yenye maji yameundwa katika mahusiamo na mwingiliano wa viumbe hai vikiwemo wanyama na mimea ya majini na kimoja kikiathirika kinaathiri na kingine. Hivyo, tunajukumu la kulinda maeneo haya yasifikiwe na kuharibiwa kwa sababu yanaweza kuhatarisha ikolojia ya eneo husika.

Zifuatazo ni sehemu ambazo huathirika zaidi na madhara ya mafuta au mafuta machafu:

1. Miamba ya matumbawe ambayo hupatikana baharini katika kina kifupi ambayo ni muhimu kwa viumbe wa majini wakiwemo samaki na wanyama wengine. Miamba huwa ni vivutio na burudani kwa watalii hasa wapiga mbizi. Miamba ya matumbawe na viumbe vya majini vinavyoishi ndani na karibu na maeneo ya pwani viko hatarini zaidi kutokana na kukosa oksijeni na kuathirika na dutu zenye sumu ndani ya mafuta.
2. Mchanga kwa kawaida huwa una uhalisi wa kujisafisha wenyewe ingawa mafuta yanaweza kuchafua viumbe na mlolongo wa chakula kwa viumbe katika mchanga.
3. Maeneo ya fukwe za maziwa au bahari ambayo kwa kawaida hayana mawimbi makubwa mafuta husambaa haraka na yanaweza kubaki juu ya fukwe kwa miaka na kuathiri mifumo ikolojia ya eneo husika.
4. Maeneo ya ziwa na bahari yenye mawimbi kidogo, kwa kawaida huwa na utajiri wa bioanuai itokanayo na jamii za mimea, wanyama na ndege. Mafuta yakifikia maeneo hayo hutuama juu ya maji na baadae kuzama kama tope na kukaa chini ya maji. Mafuta hayo yaweza kubaki juu ya fukwe au chini ya maji kwa miaka na kuathari ikolojia ya eneo hilo.
5. Mazao ya baharini kama mabwawa chumvi, mwani n.k ambayo hupatikana katika pwani huweza kuathirika na mafuta na kupelekea kuharibu ubora wake kwenye mlolongo wa chakula.
6. Misitu ya mikoko ni makazi ya viumbe mbalimbali na kuwa ni chujio la maji. Mikoko ina mizizi mirefu, ambayo hushikilia vizuri juu ya usawa wa maji na kusaidia kushikilia ardhi dhidi ya mwomonyoko wa fukwe. Mizizi hii ikizingirwa na mafuta huweza kusababisha mikoko kufa na mfano ni kama mikoko iliyopo maeneo ya fukwe za bandari ya kurasini Dar es Salaam.
7. Kumwagika kwa mafuta kunaweza kuwadhuru ndege na wanyama pale ambapo yatamfikia moja kwa moja kwenye mwili, dutu zenye sumu katika mafuta uharibu vyanzo vya chakula na makazi ya ndege na kuathiri viota vyenye mayai au watoto wadogo.
8. Madhara mengine ni pale ambapo mafuta yanamwangika kidogo kidogo kwa muda mrefu na kuingia kwenye mifumo ya maji ambayo hutumika na jamii. Mfano, maji ya visima huathirika sana na mafuta na huweza kuchukua miaka zaidi ya kumi kuweza kutumika tena. Hii inaongeza gharama kwa jamii kutafuta vyanzo mbadala vya maji.

Pale ambapo kuna shughuli ambayo huwa inahusu matumizi ya mafuta na kuwa mafuta hayo pia yanaweza kumwagika, ni vizuri kuhakikisha kuna tahadhari ya kutosha ili kupunguza hatari na uwezekano wa uharibifu kwa watu, mali, na maliasili. Mafuta yanapomwagika ni muhimu kufanya uokoaji mapema iwezekanavyo ili kuzuia utawanyikaji na usambaaji wa mafuta hayo. Kwa kawaida vifaa vinavyotumika katika kudhibiti mafuta kusambaa vinauhalisia wa kujengea vizuizi na sehemu kama kwenye maji, teknolojia ya kutumia 'booms' inatumika ambayo hukusanya mafuta kwa pamoja. Teknolojia hii urahisisha zoezi la kukusanya na kuzoa mafuta na kuyatoa eneo ambalo limeathirika, na kuyahifadhi yakisubiri mchatako wa usafishaji ili baadaye yaweze kutumika katika hali ya usalama.





*Picha: Maji ya kwenye ndoo ambayo yameathirika na oil kutoka katika mitambo ya kuzalisha umeme*

# Kauli ya Mazingira Yetu












NEMC yashiriki Warsha ya wadau wa maendeleo wa mazingira katika ukumbi wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu jijini Dodoma.



Bodi ya Wakurugenzi pamoja na Menejimenti ya Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) wamekamilisha ziara yao Mkoani Dodoma kukagua uzingatiaji wa Sheria ya Mazingira katika ujenzi wa Reli ya kisasa ( SGR).







National Environment
Management Council
(NEMC)
June 05, 2022
WORLD ENVIRONMENT DAY
Environment is no ones property to destroy, its everyone's responsibility to protect.
Only One Earth
#OurEnvironmentOurLife!


Kuelekea
Siku ya Mazingira Duniani
05 Juni, 2022
Bado Siku 1
Ni vyema kuweka mfumo maalumu wa kuzuia kelele (sound proof) katika nyumba za ibada, kumbi za starehe na baa ili kudhibiti kiwango cha sauti kinachozidi na kupelekea kelele chafuzi na mitetemo."
Bi. Irene John
MENEJA MAWASILIANO NA UHUSIANO KWA UMMA - NEMC


WARSHA KWA MAAFISA MAZINGIRA MKOA, WILAYA NA HALMASHAURI-DODOMA
Dodoma
04 Juni,2022
Kelele na mitetemo imekuwa changamoto kubwa katika maeneo mbalimbali Nchini, Wito wangu, kila anayehusika kusimamia Sheria na Muongozo wa kudhiti kelele na mitetemo awajibike kikamilifu ili tuweze kutatua changamoto hiyo.
"Tanzania ni Moja Tu, Tunza Mazingira"


MASHINDANO YA MAZINGIRA MARATHON
DAR ES SALAAM
12 JUNI 2022
Mbio hizi zililenga kujenga uelewa kwa jamii kuhusu kutunza na kuhifadhi mazingira, mazingira yakiharibiwa nchi kwaujumla itashindwa kuendelea. Tuyatunze mazingira kwa vizazi vya sasa na baadae.
"Tanzania ni moja Tu, Tunza Mazingira"


Kipindi
SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI
MZUNGUMZAJI


SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI
Tuepuke kuishi kwa mazoea kwenye suala zima la mazingira, tuhakikishe tunatupa taka kwenye sehemu maalumu zilizotengwa kwa ajili hiyo ili mazingira yetu yawe safi na salama.
Mhe. Jokate Mwegelo
MKUU WA WILAYA - TEMEKE
05 JUNI 2022
ZAKHEM - DAR ES SALAM
#MazingiraYetuUhaiWetu!


WARSHA KWA MAAFISA MAZINGIRA MKOA, WILAYA NA HALMASHAURI-DODOMA
04 Juni 2022
Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (OMR), akiwa kwenye picha ya pamoja na watumishi kutoka NEMC na Ofisi ya Makamu wa Rais Muungano na Mazingira baada ya kufunga warsha kwa Maafisa Mazingira Jijini Dodoma..


MAADHIMISHO YA WIKI YA MAZINGIRA
DODOMA
31 MEI 2022
Nimefurahishwa sana kwa jinsi mnavyojihusisha na shughuli za utunzaji wa mazingira chuoni hapa, hususani suala la upandaji miti na mradi wa kutenganisha taka. Niwapongeze uongozi wa chuo na wanafunzi kwa kazi nzuri mnayoifanya ya kutunza mazingira kwa maendeleo endelevu.
"Tanzania ni moja Tu, Tunza Mazingira"


Kuelekea
Siku ya Mazingira Duniani
05 Juni, 2022
Bado Siku 5
Kuelekea siku ya mazingira duniani, tunawakumbusha wadau wa mazingira kulipia Ada na Tozo za mazingira ili Baraza liweze kutoa huduma zake za kuyahifadhi na kuyasimamia mazingira yetu."
CPA Charles Wangwe
MKURUGENZI WA FEDHA NA UTAWALA - NEMC


Kauli ya Mazingira Yetu
Kudhibiti kelele chafuzi ni muhimu ili kulinda afya ya jamii na mifumo ya ekolojia kwa kuhakikisha maendeleo endelevu ya kizazi cha sasa na cha baadae.


Kauli ya Mazingira Yetu


# KATUNI


















ENEO HILI LIMEKUWA NA UKAME, ZAMANI HAIKUWA HIVI, PALIKUWA NA RUTUBA NA MAJI YAKUTOSHA YALIPATIKANA
LAZIMA KWA PAMOJA TUCHUKUE HATUA KUYA-LINDA MAZINGIRA YETU, VINGINEVYO HATUTABAKI SALAMA
HAYA YOTE NI MATOKEO YA UHARIBIFU WA MAZINGIRA


UKAME TULIONAO UMESABABISHWA NA UHARIBIFU WA MAZINGIRA
TANGU MWANZO TUNGECHUKUA HATUA DHIDI YA WANAOHARIBU MAZINGIRA HAYA YASINGETUKUTA
MCHORAJI: Musa Ngarango Jr.


WAMILIKI WA SEHEMU ZA STAREHE NA MAENEO YA IBADA WANAPASWA KUZINGATIA NA KUFUATA MAELEKEZO YA KIBALI KINACHOTOLEWA KWA KUZINGATIA MUDA ILI KUPUNGUZA KELELE CHAFUZI


JUNI 07, 2022
TUEPUKE UHARIBIFU WA MAZINGIRA KWA KUTOKUANZISHA SHUGHULI ZINAZOHARIBU MAZINGIRA YETU NA KULETA ATHARI ZA KIAFYA, USTAWI NA UHARIBIFU WA MIMEA NA MAKAZI YA WANYAMA. KUTUNZA MAZINGIRA NI WAJIBU WETU


KUPATA MAJI IMEKUWA TABU, KILA NINAPOCHIMBA NI PAKAVU, HII NI BALAA!
SHIDA YOTE HII IMELETWA NA WAHARIBIFU WA MAZINGIRA, KOSA LETU TULIKAA KIMYA, SASA LAZIMA TUCHUKUE HATUA KULINDA MAZINGIRA YETU


MAJI NI MUHIMU KWA VIUMBE VYOTE DUNIANI IKIWEMO SISI BINADAMU
WANAOHARIBU MAZINGIRA KWA KUKATA MITI HOVYO WANAHATARISHA UWEPO WETU, MAANA BILA MAJI HAKUNA UHAI


HII NI HATARI, TUMEENDA UMBALI MREFU KUTAFUTA MAJI NA BADO TUMEYAKOSA
WANAOHARIBU VYANZO VYA MAJI WANATULEA BALAA
SHIDA HII YA UPATIKANAJI WA MAJI MIJINI NA VIJIJINI INALETWA NA WANAO-HARIBU MAZINGIRA,NI LAZIMA JAMII ICHUKUE HATUA
MCHORAJI:


NIMEFURAHI KUONA MRADI TULIOENDA KUOMBA KAZI TAYARI WAMEFANYA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA
UTARATIBU WA KUFANYA TATHMINI KWA ATHARI YA MAZINGIRA NI MZURI, UNASAIDIA SANA KUTUNZA MAZINGIRA YETU
JAMBO HILI LISIPUUZWE, MAANA BILA KUFANYA TATHMINI YA ATHARI KWA MAZINGIRA NI HATARI KWA JAMII
MCHORAJI: MUSA NGARANGO JR.




*Kwa mawasiliano zaidi;*

**Mkurugenzi Mkuu,**

**Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC),**

35 Mtaa wa Regent/Migombani, Kitalu Na. 29/30, S.L.P 63154, Dar es Salaam, Tanzania

Simu: +255 22 277 4852/4889, +255 713 608 930, Nukushi: +255 22 277 4901

Barua pepe: dg@nemc.or.tz, Tovuti: www. nemc.or.tz


#MazingiraYetuUhaiWetu

Namba ya Bure: **0800110116**

@nemctanzania

NemcTVTanzania

www.nemc.or.tz